Q4. Should the Constitution protect, security, healthcare, water, education, shelter, food and employment as basic rights for all Kenyans? I am suggesting yes because like water is very essential, it is an essential asset, education is very important because our aim is to educate at least every Kenyan by in the near future, shelter for all is an important aspect, food, security and another thing like un-employment allowances should be in place for those who are not employed and actually have gone to school.

Q5. Who should have the responsibility of ensuring that all Kenyans enjoy basic rights such as security, health care, water, education, shelter, food and employment? I think by an act of Parliament we should have something like an Ombudsman, a local office which is neutral rather to see unto this need.

Q6. What specific issues in security, healthcare, water, education, shelter, food and un-employment should the Constitution deal with? Water for all, security, freedom of education, free education either up to Form Four because most of the parents cannot afford with the aim of educating most of the .....Kenyans not necessarily to be employed but to have general education. Food security, like the government can provide money for local stores, Cereal Boards, we can be sending our maize, our products there and we have cash money because our production may be minimal rather you cannot afford to get to the nearest district centers. So, I am suggesting we should have local stores for food security for all.

Q7. Should the Constitution provide for compulsory and free education? Yes, the government already has tried up to primary level but it should think of putting it up to "O" level.

Q8. Should the Kenyans have the right to access information in the possession of the State or any other agency or organ of the State? I am suggesting yes, all freedom of information like when the government is intending to do something, let us say, it should have a Ministry of informing the people to be informed, not necessarily to act but to have the information, information is very important for a healthy nation.

Q9. Should the Constitution guarantee all workers the right to trade union representation? I think it is yes. Thank you, that is all I can say for now, the others are written.

**Com. Phoebe Asiyio:** Thank you very much, there is a question here by Pastor Ayonga.

**Com. Pastor Ayonga:** Mr. Mbayi, you very well know that our economy is bad and since morning you have heard people saying, we want to have free education for our children. Now you have added that there should be an allowance for un-employed people, with this kind of bad economy, how much do you want this allowance for un-employed people to be and who are these because you would find that a good number of Kenyans, millions of Kenyans would tell you, I am not employed but they eat, they have shelter, they dress but they will tell I am not employed because employment means working in a school, working an office and yet those who are working on their small farms and some who are sitting by the road sides who are not working would want to be given this money. Did you take thought, who should be given this allowance and how much?

**Benjamin Kioko:** Yes, I said those like we have several graduates around who are not employed.

**Com. Pastor Ayonga:** So, it should be graduates.

**Benjamin Kioko:** Yes, they should be restricted to a certain allowance to maintain them because they are people who have used a lot of money to acquire the education or else we have others below them who have diplomas, they need to be maintained by the government.

**Com. Pastor Ayonga:** So the diploma and the graduates should be, not others below that and how much.

**Benjamin Kioko:** At least about Kshs. 5,000/= can do.

**Com. Kangu:** I take it that you take unemployment to be a problem in our country, why don't you then make some proposals on how we can create employment instead of just paying allowances to those who are unemployed. How do we restructure our system to be able to create employment for these people?

**Benjamin Kioko:** Yes, I am of the suggestion that, those who have qualified in different areas like in agriculture and are not employed should be assisted by the government to come into the play ground which is the firms and try and do something to educate the people. Let us say like charitable work, they do it without expecting much income but to educate the people how an income can be made because our country has a lot of potential in agriculture but the graduates in agriculture are doing nothing in the offices in Nairobi, they are just sitting there and they are leaving the local or rather the less trained people in the local office around the people. So, I think much is not being done and a lot of potential can be gotten out of the agricultural sector, thus we can create more employment.

**Com. Phoebe Asiyo:** Thank you, I just have one question, you said that only those who have had education should be given some monthly allowance, I thought you wanted to say that they should be given some small loans to start either that farming that



you are talking about or some business because anything that is free, like when you get a free newspaper you do not normally read it, you do not value it. At the same time there are people who work very hard like women, they start very early in the morning and they go to bed very late. May be they work even harder than the graduate you are talking about, should they also not be considered for some payment if you are going to pay people who are not earning?

**Benjamin Kioko:** Yes, I think I had forgotten that one, I should have considered that but you have helped to put that point straight. Those people like the women should be assisted in any way by the government by being given some funds, let us say to do some agricultural work or social like making pullovers, like buying the machines needed. That is a point to add to my suggestions.

**Com. Phoebe Asiyo:** I hope there are no other questions, Mr. Kioko, I want to thank you very much, please go to that table and sign our register and also leave your memorandum with us. Now I call upon Mr. John Kilonzo, I think you would have to come here Bwana Kilonzo otherwise we cannot record you and we want to hear you well. You can come to the front and stand there. Kuna kitu ambayo inanishangaza sana hapa, naona kila mtu anaongea kwa Kizungu tu, sijui kama watu wengine pia wanafahamu, tusiwe Wazungu, tuwe Wakamba na Waswahili, tuongee kwa lugha yoyote ambayo mtu anataka kuongea. Kama mnafikiri Kizungu ndio sisi tunasikia itakuwa na bahati mbaya, mtu aongee kwa lugha yoyote ile anataka, Kikamba, Kiswahili na Kizungu.

**Speaker:** Umefanya vizuri kufungua nafasi ili waongea na Kiswahili maanake wengi wa wazee hapa hawajui Kizungu.

**Johnes Kilonzo:** Thank you Madam Chairlady and the other Commissioners of this Commission. Yangu nitaongea kwa Kiswahili kwa vile nimesikia wakati huu Kiswahili ndio inatakiwa na wetu wengi hapa. Nilikuwa nimeandika kidogo hapa kwa Kizungu lakini nitaipindua kwa Kiswahili.

**Com. Phoebe Asiyo:** Umesema umeandika.

**Johnes Kilonzo:** Sijaandika yote lakini nilikuwa nimeandika kidogo kidogo. Yangu nitaanza na mambo ya hii Commission.

**Com. Phoebe Asiyo:** Sema jina lako tena?

**Johnes Kilonzo:** Johnes Kimatu Kilonzo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Johnes Kimatu Kilonzo, haya endelea Bwana Kilonzo,

**Johnes Kilonzo:** Nitaanzia na hii Commission ya Constitutional Review, nyinyi mko hapa, hii Commission ningetaka maoni

yangu iwe permanent, hii Kenya Constitution iwe permanent iwe na review laws after every 20 years.

**Speaker:** Endelea.

**Johnes Kilonzo:** Serikali, tuwe na serikali ya kiraia kama ile pia tuko nayo leo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Endelea tu na vile umeandika.

**Johnes Kilonzo:** Ya tatu, tuwe na Rais na Prime Minister.

**Com. Kangu:** I think you can use English.

**Johnes Kilonzo:** Hapana tuendelee tu kuna watu wengi hapa hawasiki hiyo, nataka wasikie kile ninasema.

**Com. Pheobe Asiyo:** Unataka tuweke President tena tuwe na Prime Minister, haya endelea.

**Johnes Kilonzo:** Members of Parliament wawe wanachaguliwa vile wanachaguliwa wanakaa 5 years lakini wawe na kazi wamepatiwa na raia kwa vile wanatuhidi mambo tano, wanahaidi watu wamewachagua vitu tano, kwa hiyo miaka tano na wakikosa kutimiza hizo vitu amesema wawe wanapelekwa kotini na wananchi baada ya hiyo miaka tano, wanashtakiwa.

**Com. Pastor Ayonga:** Endelea.

**Johnes Kilonzo:** Pia ma Councillors wawe wanakaa kwa hiyo miaka tano na ile kitu wanaahidi wananchi, wananchi wanaandika wanapeleka kwa serikali na wakikosa kutimiza pia wanapelekwa kwa koti, wanashtakiwa. Kwa vile wengi huenda kulala na mambo mingi hapo..... *(Incomplete)*

**Com. Phoebe Asiyo:** Endelea.

**Johnes Kilonzo:** Urais, raia wa Kenya awe anatambulika na kabila. Kama mtu, kwa vile tunajua hakuna Mkamba wa Tanzania, hakuna Mkikiyu wa Uganda awe anaangaliwa yeye ni kabila gani. Ikiwa ni mmoja wa kabila za Kenya 42 vile wako awe anaitwa mraia wa Kenya.

**Com. Phoebe Asiyo:** O.K. endelea.

**Johnes Kilonzo:** Haya, tuwe na administration lakini Chief awe ndio wa mwisho kwa administration na awe elected by the

people.

**Com. Phoebe Asiyu:** No D.O. DC na PC?

**Johnes Kilonzo:** From PC, DC, DO to Chief only.

**Com. Phoebe Asiyu:** Hakina Sub Chief.

**Johnes Kilonzo:** Ndio, lakini Chief awe elected na people.

**Com. Phoebe Asiyu:** Umesema hivyo, endelea tu. Kama umeandika na imepotea unaweza patiana hiyo karatasi pale kwa meza halafu mwingine naye apate nafasi ya kuongea. Kuna swali hapa ambayo tunataka kukuliza.

**Com. Pastor Ayonga:** Bwana Kilonzo, umesema MP wako akienda huko parliament na yale mambo alisema atafanya asipofanya ashtakiwe? Kama alienda na akasema mimi nitapasua bababara kutoka hapa mpaka pahali fulani halafu akienda huko parliament anaambiwa hakuna pesa na anasema anataka pesa, unaona kutaka kwake hajafanya makosa lakini parliament imepata hakuna pesa na yeye hajatengeneza hiyo barabara. Ukimpeleka kotini, koti itamfanyia nini?

**Johnes Kilonzo:** Basi naye akiitisha kura asiwe anahaidi watu zile impossibilities kwa vile sasa hata watu wamekosa imani na hawa watu wamechaguliwa, wanasema tumechagua mtu na ameenda kulala Bungeni, tumechagua mtu na hakuna kitu anatumfanyia kwa hivyo aahidi watu, ata ikiwa unawaambia, nitachimba mtaro hapa, ile kitu unajua wewe hata serikali ikikosa pesa utachukua jembe ukachimbe hiyo mtaro waone kama kweli umefanya kazi. Zile vitu umeahidi, uahidi zile vitu unaweza, sio zile vitu za kudhania.

**Com. Pastor Ayonga:** Unataka kumaanisha ya kwamba mtu atakapo kuwa anataka kura lazima aandike na wapatane na constituency yake na hayo mambo yaandikwe chini na aahidi?

**Johnes Kilonzo:** Zile vitu anaambia watu, awaambie ile kitu anaona anaweza.

**Com. Pastor Ayonga:** Lakini asipoweza?

**Johnes Kilonzo:** Asipoweza baada ya 5 years.

**Com. Pastor Ayonga:** Apelekwe kotini.

**Johnes Kilonzo:** Apelekwe kotini ashtakiwe.

**Com. Pastor Ayonga:** Si umyime kura badala ya kumpeleka kotini.

**Johnes Kilonzo:** Alisema ataweza, alituambia ataweza.

**Com. Phoebe Asiyu:** Wacha nikusaidie kidogo, nchi zingine kuna kitu kinaitwa sheria ya kuitisha yaani rule of recall, kama ameonekana alichagulia nyuma muda ya miaka mbili, tatu hajarudi nyumbani, hajafanya kazi yoyote, wananchi wanaweza kukaa pamoja kwa hiyo Constituency wakatengeneze wakapata signature ya watu wengi na kuenda kwa Speaker kwamba huyo harudishwe halafu uchaguzi ufanywe, hii imefanyika kwa nchi zingine hawajapelekwa kotini.

**Johnes Kilonzo:** Ata hiyo ni mzuri, hiyo umenisaida, uniandikie hiyo ni nzuri.

**Com. Phoebe Asiyu:** Asante.

**Com. Kangu:** Wewe umesema uraia wa Wanakenya uwe unafuatana na makabila ya Kenya lakini mimi niko na tashwishi kidogo kwa mfano yale makabili ambayo yanaungana na nchi kama mbili au tatu, kwa mfano upande wa Somalia tuko na Wasomali upande wa North Eastern vile vile tuko nao nchini Kenya, tuko na Masai Tanzania, tuko na Wamasai Kenya, tuko na Wateso ndani ya Kenya, tuko na Wateso upande ya Uganda. Unanielewe hiyo maneno, ata iko Baluya upande ule na upande huu. Sasa tunauliza wewe maneno kama haya tutafanyaje?

**Johnes Kilonzo:** Sasa vile iko, siwezi sema mimi ni Mganda na niko na kitambulisho ya Kenya, hiyo nilikuwa na sema wakati ata Polisi anaitisha mtu kitambulisho awe ana-consider kabila, anajua hiyo kabila iko Kenya au haiko Kenya, ikiwa iko Kenya ajue hiyo ni kitu ya mbele aniwekee right kwa vile hiyo kabila iko Kenya. Sikuwa nasema kuwa kabila uwe na kitambulisho ya Kenya na wewe ni wa kabila ambayo si ya Kenya lakini kitambulisho uko nayo.

**Com. Kangu:** Hapana, mimi nasema hivi, Wamasai ata kama ukiangalia upande wa Masai, wako Tanzania na wako Kenya, umenielewa? Na kuna zile makabila kama Wasomali wako Somali na wako wapi? Kenya tunaielewana, na kuna vile vile Waluhya wengine wako Uganda na wengine wako Kenya sasa kama Mluhya anatembea na ID, apewe uraia mara moja  
.....(Inaudible).

**Johnes Kilonzo:** Hiyo nilikuwa nasema kwa vile Kenya iko na kabila nyingi kama vile tunajua wako wengi, nilikuwa nasema kama hawa hawawezi fika kabila saba, ni kama kabila wanne au tano. Hiyo iwe na Constitution, ile kabila mingi sana kwa zile makabila ya Kenya.

**Com. Kangu:** Iwe inaangaliwe kwanza.

**Johnes Kilonzo:** Kuna kitu ingine nilikuwa nimesahau, excuse me, nilikuwa nimesahau na kitu important, mambo ya chama tafadhali ata ndio ilikuwa ya mbele.

**Com. Phoebe Asiyo:** Sema basi.

**Johnes Kilonzo:** Vyama mimi nasema iwe mbili, vyama mbili tu, ata Yesu aliwacha njia mbili ya kuenda mbinguni na kwa shetani kwa hivyo vyama viwe mbili, ikiwa chama moja ni ya kupeleka watu mahali pazuri ipeleke ikiwa ile ingine ni ya kupeleka kwa shetani ipeleke kwa shetani, ni chama mbili tu.

**Com. Pastor Ayonga:** Hebu ni ku-correct kitu kimoja, Yesu hakuwa na njia mbili alikuwa na njia moja tu, hakuwa na njia mbili.

**Johnes Kilonzo:** Alituambia njia ni mbili.

**Com. Pastor Ayonga:** Ndio lakini hakutuletea njia mbili ya pili ni wewe mwenyewe unachagua, yeye alikuwa na njia moja ya kuchukua watu pahali pamoja hiyo ingine ni wewe utachagua.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante.

**Johnes Kilonzo:** Mimi nasema hiyo juu ya chama kwa vile, sasa hiyo imekuwa kitu ingine, vyama mingi imekuwa mingi mpaka tunakuja kuona kama kila mtu atakuwa na chama chake na bibi yake kwa vile chama ikiwa vile inaendelea zitakuja kuwa 30 million na zikiwa 30 Million kila mtu atakuwa ya yake na bibi yake na hakuna mtu atapatia mwingine kura kila mtu atakuwa na bibi yake watu wawili, kwa hivyo chama mbili tafadhali utuandikie hapo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tumekusikia vizuri, hebu andika jina lako hapo, tuko sana na Bwana Mutuku Mbwika, simama pale, Bwana Mutuku useme jina lako sawasawa kabisa ili tuandike vizuri na uongee kwa muda wa dakika tano tafadhali.

**Mutuku Mbwika:** Naweza kuongea lugha gani? Naweza kuongea kwa Kikamba?

**Com. Phoebe Asiyo:** Ongea kwa Kiswahili ni mzuri.

**Com. Pastor Ayonga:** Ili tukusikie.

**Mutuku Mbwika:** Nashukuru kwa.....kwa sababu hii nchi yetu inaonekana ni nzuri sana kwa vile nchi mingi iko na taabu na hii nchi yetu ni nzuri. Nimeshukuru kwanza kwa President wetu na kupatiwa nafasi ya kutoa maoni yetu, hapo tumeshukuru na kwa wananchi ambao wamekuja hapa vile vile nawasalimu. Mimi maoni yangu si mengi sana.

**Speaker:** Sema jina yako.

**Mutuku Mbwika:** Jina langu naitwa Paul Mutuku.

**Com. Kangu:** Zungumza tu ukituangalia kwa sababu tuna-recordi maneno yako.

**Mutuku Mbwika:** Mimi naongea kwa upande wa sheria kama inawezekana. Kwa hivyo haya ni maoni yangu, ningependa kusema kuhusu mambo ya President naweza kubaliana nayo, PC, DC, DO, Chief na Sub Chief kwa sababu tukikosa watu kama hawa tunaweza kuharibu mambo mingi sana katika villages. Kwa sababu Chifu inaonekana hawezi kutembea kwa village yote yeye analinda location kubwa, lazima awe na msaidizi wake kama Sub Chief / Assistant Chief ndio anaweza kushika wale wanaharibu vitu na kuwapata kwa urahisi lakini Chifu akiwa pekee yake tutakuwa na shida kwa hivyo mimi naomba serikali yetu hapo iangaliwe kwa imani.

Ile ingine nataka kusema, hii sikuandika ni mambo ya kisomo, hii tumefanyiwa vizuri sana na serikali kupatiwa bure kutoka Seven mpaka Eight lakini kuna taabu moja inatusumbua wazazi kwa sababu hapa reserve kwetu watu wengi ni wakulima na saa zingine wanalima na mazao haipatikani, mvua inapotea ata mnajua sasa wakati watoto wanasoma shuleni kuna wakati tunataka kujua serikali sheria wanaweka kwa masomo, kwa sababu wakati wamefunga shule, kuna watu wengine wanafanya tuition na hiyo tuition inategemea pesa na watu wengine hawana pesa, ningependa kama shule unafungwa zamani shule ilikuwa inafungwa na watoto wanaenda nyumbani?

Ikiwa ni contract, kama mambo ya tuition wale ambao ni senior retired teachers yaani waweke shule yao kando ili wasomeshe watoto wakati wa tuition, ndio yule mzazi ambaye hana pesa, mtoto wake akirudi kwa shule asifukuzwe kwa sababu mtoto akikosa kutoa pesa ya tuition akirudi shuleni anaweza kufukuzwa na hii ni taabu inasumbua watoto kwa sababu sisi hatuna mapato. Kwa hivyo tungependelea serikali iamue tuwe na shule ya senior teachers wale wame-retire wapatiwe shule yao kando ama wawe na shule yao kando ndio mtu akitaka kupeleka mtoto wake kwa prep / tuition apeleke pake kwa sababu hiyo ni contract. Lakini shule ikifungwa naomba serikali ifungwe kabisa kwa sababu zote zinafungwa, wale wanapesa wapatiwe nafasi ya kupeleka watoto, sio watu watu wote, hatuna pesa, sasa hiyo itakuwa ni shida kwa sababu mtoto akienda anaambiwa atoe pesa ya prep na mimi sina, taabu iko hapo kwa hivyo serikali ikiwa na msimamo moja na kuamua kila kitu hii nchi yetu itakuwa nzuri hakuna mtu atapigana na mwingine. Yangu ni hayo tu si mengi.

**Com. Phoebe Asiyu:** Asante sana Bwana Mutuku nafikiri mambo yako tumeyafahamu Sijui kama kuna swali lolote kwa

Bwana Mutuku. Asante, tafadhali fika pale uandike jina lako kwa register yetu na kama una karatasi uache hapo. Sasa ningependa kumuita Bwana B. M. Kitaka, tumefurahi umekuja kwa vile kuna watu wengine wanafanya kazi ya serikali na hawataki kuja hapa kutuambia mambo ya serikali. Hatujaona Chifu hapa ameleta habari yake au Assistant Chief, kwingine tumeenda wametueleza mambo na hapa hatujawaona. Muende muwambie wawe wakija hapa wakitueleza habari maana wengine wamesema wafutwe sasa wangetuambia wakiwa hapa wasifutwa, wajitetee, muwaambie hivyo, wasikose kuja hapa. Asante Bwana Kitaka sasa tumekupa nafasi.

**B. M. Kitaka:** Commissioners na wananchi kwa jumla, mimi naitwa Boniface Mboga Kitaka, na mimi ni mfanyi kazi wa serikali (civil servant).

Maoni yangu nitapeana inform of points halafu kama kuna swali nitaulizwa. Mimi nitaanza na hali ya wazee, watu ambao wana-retire kutoka kazi ya serikali na wale wanakuwa retrenched. Ninapendekeza, wale watu wanafikisha miaka hamsini na tano, waki-retire walipwe marupurupu yao mara moja bila kungojea kwa sababu tumeshaona wengi wamepatiwa retire wanangojea mwaka moja, miaka miwili halafu familia na watoto wanafukuzwa shule na wanahama, kwa hivyo Katiba iandikwe, kama mtu ameshafanya kazi ya serikali na amepewa retire, marupurupa yawe tayari aende nayo.

Nikiwa hapa hapo tu, kuna watu wengine walipatiwa ile retrenchment / early retirement, wengine wako na miaka thelathini, wengine wako na 40 hata wengine wako na twenty something. Napendekeza Katiba iandikwe, kama mtu anakuwa-retrenched kwa sababu si kupenda kwake, NSSF imlpe ile pesa yake mara moja bila kumwambia angojee miaka hamsini. Kwa sababu tumeshaona huko vijijini, watu wengi wa aina hiyo walikuwa kazini, wamekuwa retrenched ama wame-retire na kuna shida nyingi ata watoto wamefukuzwe shule kwa hivyo, hiyo ingewekwa kwa Katiba.

Ingingine ni juu ya urithi (property/land), sijui kama ni hapa kwetu Ukambani lakini pengine makabila mengine Kenya. Mwanamke harithi. Niko na maoni; kama watoto wamezaliwa na baba mmoja, wasichana na wavulana na kuwe na msichanani moja au wawili hawajaolewa na wako na watoto, iandikwe kwa Katiba, awe akipatiwa property agawanywe pamoja na brothers asiachwe huko kama mwombaji, kwa hivyo awe na right to own the father's or the parent's property.

Ile ingine ni maoni yangu kwa uchaguzi; wakati wa uchaguzi tunakuwa na kazi nyingi ya kuchagua Councillor, MP na President. Ni maoni yangu Katiba ya Kenya ipinduliwe, kuwe na wakati wa Councillor na MP na kuwe na wakati wa President pekee yake ili sisi sote tu-concentrate huko na tuwe tunachagua bila kutatanishwa. Kwa sababu tumeshaona Councillors wengi, MPs wengi wamepita kwa sababu wanaunga President, sio ati ali-campaign sawa sawa lakini kwa sababu wa mfumo tu, kwa sababu yule anaitisha Presidency anampenda hata wanampigia mwingine Mjumbe, wanapigia mwingine Councillor ambaye hana uwezo kwa hivyo tuwe na wakati wa kuchagua President peke yake.

Ile ingine, ningependekeza kama mfanyi kazi ya serikali, sisi watu wa serikali tumeumia sana juu ya mshahara. Kwa hivyo ni

maoni yangu Katiba iandikwe kuwe na Tume maalum ya kuchunguza mishahara na marupurupu ya wafanyi kazi wa serikali after every 2 years badala ya kunjojea wakati wanasisia watapendekeza wapewe kiasi fulani, kwa hivyo kuwe na tume specifically to review civil servants' salaries.

Ya mwisho, ningetaja kidogo kuusu Provincial Administration. Ni maoni yangu Provincial Administration ama Utawala wa Mkoa uweko, let it be there to stay kwa sababu kama hakuna utawala kutoka juu mpaka chini, uongozi hautaendelea. Kukosa kuwa na Assistant Chief, Chief, DO, DC, ni kama kichwa ambacho hakina miguu kwa hivyo ni lazima kuwa na President na kuwe na chain of authority kutoka top mpaka bottom. Kwa vile watu wengi wakisikia hii jina Chief, Assistant Chief, DO ama DC wana ile mentality ya ukolini hapo zamani, walikuwa wamechaguliwa na mkoloni na wanaletwa mbele na ni watu hawakuwa wamesoma, kwa sababu siku hizi, Chiefs and Assistant Chief wamesoma na ni watu wame-attend courses, na wanafanya kwa other ministries, they should be seen as civil servants but not the colonial rulers ama watu wa "himla" watawala wa "himla". Na kama kuna mmoja Chief ama Assistant Chief ako na makosa yeye aingiliwe kiviake lakini tuwache kujumulisha ati utawala wa mkoa ni mbaya. Ma-Chief na ma-Assistant Chief wale wako siku hizi, karibu wote wamemaliza form four na wamesoma na watu, kwa hivyo ni maoni yangu, iendeleo na kukaa lakini kuwe na watu ambao wamesoma na wawe wanapelekwa seminars ili wajue vile wataishi na watu wao.

Hii maneno ya let us do away with Provincial Administration, it is the language of the opposition and I know they say that because they are not ruling, when it their turn to rule will come (*sorry nimeruka*). Nasema hii lugha ya kusema utawala wa mkoa uvunjwe ulitokana na upinzani kwa sababu hawatawali, lakini wakati wanatawala wakalie kiti, watajua huwezi kutawala ukiwa uko juu na hakuna chain, hakuna kitu kinashikanisha kutoka juu mpaka chini, kwa hivyo I say let the Provincial Administration stay and let us have education people and if possible, kama inawezekana, kama ni Assistant Chief waandikwe kama waalimu na wawe transferred from location to location. Tuseme hata kama si Kenya mzima, kama ni hapa Machakos kwa sababu Chiefs and Assistant Chiefs wanaenda kufanya interview kwa DC, wawe transferred within the district, itakuwa mzuri na wawe kama civil servants kama waalimu na wengine. Kwa hivyo kwa ufupi hayo ndio maoni yangu, asante Commissioners.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tumeshukuru sana sana Bwana Kitaka, lakini kuna swali moja kutoka kwa Pastor Ayonga halafu Doctor Maranga.

**Com. Pastor Ayonga:** Bwana Kitaka umeongea juu ya urithi wa wasichana kwamba wawe na haki ya kupewa property.

**B.M. Kitaka:** Kama hawajaolewa.

**Com. Pastor Ayonga:** Sasa kama hakuolewa ya Mungu ni mengi, kesho ikitokea huyu msichana akapata mume, what happens na hii property aliyopewe hapa kwa baba yake sasa ameolewa upande ingine, hiyo hukutuambia?



**B. M. Kitaka:** Hata enda nayo uko if ..... wale wamebaki kwa hiyo boma, akiolewa ana forfeit the right to inherit.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na kama kule aliolewa huyu kijana hawana shamba kwao.

*(Murmur)*

Ni kweli, msichana ameolewa kama baba yake amampatia kashamba kadogo na ameolewa na kijana yule hana shamba hata kidogo kule kwao, atakaa na njaa huko?

**B.M. Kitaka:** Vile naona, kama hawana uwezo wa kununua shamba yao, kwa sababu wote ni watoto, kama ni msichana wangu ameolewa na nampenda na napende yule ememwoa, kama niko na big piece of land, lakini hiyo isiandikwe...*(Laughter)* ) waje waongee na mimi.

*(Interjection)*

**Com. Pastor Ayonga:** Ati isiandikwe?

**B.M. Kitaka:** Isiandikwe kwa Katiba, mimi nasema Katiba wakati huu isiandikwe huko, arudi kwa baba yake na son-in-law na sister waje waongee na baba watafutiwe namna.

**Com. Pastor Ayonga:** Unasema hiyo inakuwa katika un-written Constitution, unasema mambo ya namna hiyo yanakuwa katika un-written, si hii yetu tunayoenda kuandika lakini ile ya kufahamiana kwamba mtoto wangu ameenda kwa fulani na hawana kitu, atarudi mimi nitampa kitu. Hiyo haikuandikwa, si ndio?

**B. M. Kitaka:** Iandikwe, kama huko wana shida iandikwa waje kwa wazazi wao, na wataketi iangaliwe.

**Com. Pastor Ayonga:** Mambo yaangaliwe.

**Com. Phoebe Asiyo:** Lakini ya muhimu, wewe umesema watoto wote vijana na wasichana kama wasichana, hawajaolewa baba awapatie ardhi. Asante sana hiyo ndio yako.

**Com. Kangu:** Nikifuatilia hilo, umesema ikiwa msichana anaolewa shamba inarudi igawe kwa ndugu zake. Ikiwa anapatiwa shamba, anafanya development, tuseme pengine ni plot hapa Muuma Andu, amejenga manyumba zake na pesa zake, sasa hii irudi kwa ndugu zake ama itakuwe namna gani?

**Com. Phoebe Asiyo:** Msichana hajaolewe amejanga nyumba.

**Com. Kangu:** Na baadaye anaolewa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Halafu anapata bwana.

**Com. Pastor Ayonga:** Hta ana shamba la kahawa ambalo amekuwa akichuna kahawa kila wakati.

**B. M. Kitaka:** Kama huko ameolewa kuna shida hawana kitu, tunaweza pindua tuseme msichana aoe.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na hiyo nyumba yake amejanga?

**B. M. Kitaka:** Hapana, nasema msichana ana mali hapa kwa baba yake na kule anaolewa hakuna mali, wacha huyo msichana yeye mwenyewe atoe huyo mwanamume waje kukaa hapo.

**Com. Maranga:** Kimila je, wacha nikulize, mila ya Wakamba inakubali hiyo kweli? Hiyo ni uwongo.

**B. M. Kitaka:** Haikubali hiyo, lakini hatuweze kuwa tied na kimila, kama mambo ni mbaya itakuwa mbaya, huenda ikawa Kikamba inasema namna hiyo lakini watu wamepinduka na wakati kwa hivyo inaweza pinduliwa.

**Com. Maranga:** Niko na swali mbili, ya kwanza kabisa ulisema kura za Rais na ya Wabunge zifanywe siku tofauti, mimi nauliza ni gani inatakiwa ifanywe kwanza na ni wakati gani kati ya Rais na zile zingine, mimi nataka muda gani unafikiria, ni gani inafanywe mbele, ni ya Rais ama ni ya Councillors na Wabunge? Ni gani unaona ije kwanza kwa mafikirio yako? Hiyo ni swali la kwanza.

**B. M. Kitaka:** Kwa maoni yangu ninaonelea tuchague Councillors na Wabunge halafu baadaye tuchaguwe President.

**Com. Maranga:** Wakati gani kati ya hiyo na hiyo ingine, mwezi moja, siku saba ama nini, ama wakati gani?

**B. M. Kitaka:** May be after something like 6 months.

**Com. Maranga:** After 6 months.

**Com. Phoebe Asiyo:** No, hiyo si kweli, hiyo miezi sita unasema nchi itakaa bila President na iko na Wabunge na Councillors halafu nani ataongoza serikali?

**Com. Marang:** Hiyo ni maoni yake mama.

**Com. Phoebe Asiyo:** No, No.....(*inaudible*)

**B. M. Kitaka:** Wacha niulize kama December tutaenda kwa uchaguzi, President atakuwa ametoka kwa kiti ama atakuwa kwa kiti?

**Com. Phoebe Asiyo:** Siku ya President ikifika, according to the present Constitutiton, the life of the President in office expires on the 5<sup>th</sup> of January next year, unasema kwamba yeye akaye miezi sita zaidi tuingojea kuchagua president mwingine?

**Com. Kangu:** Swali ni transitional arrangement?

**B. M. Kitaka:** The ..... (Inaudible) kwa sababu.....

**Com. Phoebe Asiyo:** Untill a new President is put in place?

**B. M. Kitaka:** Because ata kama kuna uchaguzi, yeye anaendelea na kazi kama President.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na kwa nini akae miezi sita kama kabla ya uchaguzi ya President ingine, kuna sababu ya hiyo?

**B. M. Kitaka:** Hayo ni kwa maoni yangu na mngerekebisha vile mnaona ama ..(*Incomplete*)

**Com. Maranga:** Swali la pili?

**Com. Phoebe Asiyo:** Another question?

**Com. Maranga:** Wewe unasema provincial administration ibaki na iendelee, kitu mimi nakuuliza, wewe unatosheka vile PC, DC, DO, Chief na Assistant Chief wanachaguliwa, unatosheka?

**B. M. Kitaka:** Vile wanachaguliwa, mimi nasema wameandikwa kama civil servants wale wengine natosheka, lakini mtu akiwa mbaya achukuliwa sheria kivyake.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana, nimeshukuru Bwana Kitaka. Sasa ningependa kuuliza Mbithi Kala. Mbithi nimefurahi wewe ni mama na umechagua kuongea na sisi. Ningependa kuuliza akina mama wote walio hapa, kwa maana ni wachache wapange fikira zao na waongee na sisi leo, kwa maana wanaume wote wameongea mmoja tu aliongea habari ya akina mama na alisema

kabisa wachaguliwe kwa Bunge wapigane tu na wanaume ndio wapate nafasi. Lakini wale akina mama walio hapa tafadhali tunataka muongee, wale watu ambao hawajiwezi muongee, wale vijana walio hapa tafadhali muongee ili tupate Katiba iliyo na fikira ya watu wote, wale walemavu, wale vijana na akina mama. Haya sasa Mbithe endelea tafadhali.

**Muna Mbithe:** Kwa jina naitwa Muna Mbithe Kala. Mimi ni mmoja wa 3C's Machakos Constituency. Kile nataka kusema kwa maoni yangu, sorry, akina mama huko nyumba wameniambia niongee kwa lugha ya Kiswahili.

**(Interjection)** Inaudible.

Sasa mimi kwa maoni yangu, yale nataka kutoa hapa, kwanza uongozi huanzia nyumbani. Na uongozi ukianzia nyumbani, sana sana wakina mama, kwa mfano mama akiolewa kama mimi naweza kuolewa na nimalize miaka kumi hivi kama sijatolewa ile mahari ya customary law, ile mahari wanawake wanatolewa. Kwa mfano kwetu, tuna ile mahari tunatolewa ni mbuzi tatu.

**(Interjection)** Peke yake.

Hapana, ya kwanza ile Mkamba anajua, ile ya kwanza na kwa bahati mbaya naweza kufa hata nikiwa na miaka hiyo kumi na sijatolewa ile mahari. Hapo tunapata shida sana sababu gani? Nikikufa, wenye boma wanaweza kusema mimi sio mwenye boma, wanaweza kusema huyu sio wetu wa boma, na sisi tunakaa hapo hata pengine nimezaa watoto wengi, hata pengine nimezeeka kwa hiyo boma na watasema huyu sio wetu apelekwe kwao, azikwe kwao. Hiyo ni kitu moja sisi akina mama tunapata shida sana.

**Com. Phoebe Asiyu:** Pendekeza sasa.

**Muna Mbithe:** Sasa mapendekezo yangu ni kusema ya kwamba, tukiolewa kwa hiyo boma hata tukiwa na miaka mbili, iwe ya kwamba sisi ni hapo kwa hiyo boma.

**Com. Pastor Ayonga:** Mama endelea.

**Muna Mbithe:** Nikiendelea sioni ni kwa nini tunaambiwa ati tukapelekwe huko kwetu kwa sababu tumeolewa na tunafanyiwe hii, naona ata tukiwa ata miaka mbili hiyo hakika ihakikishwe huyu mama ni wa hiyo boma.

Kiti ingine, uongozi wa akina mama, sisi tunataka kuchaguliwa bila kuwa na uchaguzi ile tunakuwa na wanaume pamoja, sisi tunataka kuteuliwa kama akina mama tuwe ma-Councillors, tuwe MPs hata tuwe Chiefs na DC bila upingamizi.

**Speaker:** Bila kujali.

**Speaker:** Hajasema hivyo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Tafadhali do not put words in her mouth, give her time to say what she wants to say, please.

**Muna Mbithe:** Sisi tunataka hivi kwa sababu tunaona tukiitisha kura na hawa wanaume, saa ingine wanatutukana na sisi tunajua uwa wanawake sisi ndio wengi. Na saa ya kuitisha kura, hawa wanaume wanatutukana, saa ingine mama anashindwa nitaanzia wapi nitamalizia wapi. Hii ni kwa sababu nikisimama na Councillor mwenzangu ananitukana huyu munaona huyu ni malaya huyu ni ni, na mimi nashindwa na vile nitaendelea na vile nitaendelea na kuomba hiyo kura. Kwa hivyo ndio tunasema tutengewe vitu yetu, tuwe tukipatiwa vitu yetu bila...

Ile ingine, sisi akina mama tunazaa watoto, kwa mfano tunazaa watoto wengine vipofu, viwete na tunawalea na tukiwalea saa ingine wanaweza kupata mimba. Wakipata mimba wanaweza kupata mimba na mtu ana miguu ya kusimama, unaelewa vile nasema, anajishika hivi, na huyu akizaa naye anamwacha hata anaweza kuzaa na mtu ambaye anaendesha pajero na huyu baadaye anajificha anaenda hivi hivi, hiyo hatutaki.

**Com. Phoebe Asiyo:** Unataka namna gani?

**Muna Mbithe:** Tunataka akizaa na huyu kipofu aoe, (*Laughter*) tunataka hivyo, aoe huyo kwa sababu ni yeye alilete hiyo. Kwa sababu akiwa na hiyo mimba mama hawezi kuenda kanisa, hawezi kuenda kwa mikutano kwa sababu anaangalie huyu atazaa namna gani. Ndio sababu tunasema akipatia huyu msichana mimba ama huyu kiwete, amuo na sheria ile inatakikana.

**Speaker:** Endelea.

**Muna Mbithe:** Nikiendelea, nataka kusema ma-chifu wachaguliwe na watu. Iko sababu Chifu anaweza kaa hapa kwa muda wa miaka thelathini au hamsini na awe ama ananichukia ama anachukia mwingine, ndio tunauliza tutakaa na huyu Chifu kwa miaka hizo zote akiwa hanipendi na nakaa kwa hiyo kijiji na ni yangu na siwezi hama? Ndio hapa tunasema Chifu tunataka kumchagua kama tunachagua ma-Councillors. Ata Sub Chifu wachaguliwe na raia vile vile, tumesema.

Ya mwisho, Wajumbe: Sisi tunataka tukichagua Wajumbe kuwapeleka Parliament wasitufanyie chochote, ama hawafanyi kazi hapa kwetu hata ikiwa tunawaita tukiwafuta kazi, tuwe tukiwarudisha hapa kwa sababu hawakutimiza mahitaji yetu, yale tuliwatume waende huko watufanyie.

Nimesema Machifu wale wako hapa wanisamehe kwa sababu ni maoni yangu vile mimi naona. I

**Com. Phoebe Asiyo:** Mama Mbithe, hii ndio wakati wako pekee katika nchi hii ambayo umepewa fursa ya kusema kila kitu kilicha rohoni mwako au rohoni mwa watu wa hapa ambayo unataka irekebishwe kwa Katiba, hata kama President angekuwa hapa, ungesema tu vile unasema.

**Muna Mbithe:** Ningesema ata ikiwa nani, ningesema siwezi kuogopa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Ndio, endelea tu.

**Muna Mbithe:** Ile ingine, tunataka President na tunataka Prime Minister. Na ya mwisho ni watoto wawe equal. Kwa sababu wote ni watoto na ni sisi tuliwazaa ata naweza zaa mtoto na niwe tajiri, huyu azae maskini sisi tunataka iwe balanced. Wakipatiwa huku na huko, wawe wakapatiwe na hiyo iwe kama. (incomplete)

**Com. Phoebe Asiyo:** Mambo ya urithi.

**Muna Mbithe:** Na mimi nafika hapo.

**Com. Phoebe Asiyo:** Kuna swali kwa Doctor Maranga.

**Com. Maranga:** Mama nauliza, ulikuwa ulikuwa umesema, kulingana na kimila ya Wakamba, wanatoa mbuzi tatu, hiyo mbuzi tatu inamaanisha ndio imefungwa, si ni hivyo? Kama mbuzi tatu imetolewa basi wewe ni bibi wa ule mtu, asante. Sasa kitu nakuuliza, hiyo ulisema ati wale ambao wanapata watoto na wasichana, wengine hapa, kama watu wa pejero, na unasema walazimishwe kuo hawa watu ama hawa wasichana, sasa mimi nauliza, kama huyu mtu tayari ameoe na sheria inasema hatakiwi kuo bibi mwingine tutafanyaje, kuna njia ingine badala ya kumuoa?

**Muna Mbithe:** Sisi hatutaki, ni maoni yangu, kama mimi sitaki ati akiwa na binti wangu awe akioa huyu wangu alikuwa na mwingine, hapana. Kwa sababu si aliwacha huyo mwingine akija kuona huyu, si alimwacha akaja kwa huyu, na huyu anaona kwamba haoni hata anaona hana miguu. Sasa tunataka amue na amue na sheria ile ambayo ni sheria ya kawaida, ile ya sheria house hata ikiwa sio ya kanisa, amue.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nimeitikia hiyo, kwa hivyo unasema kwamba polygamy sio kitu kibaya kwa nchi hii.

**Muna Mbithi:** Ati?

**Com. Phoebe Asiyo:** Polygamy, tuendeleee tu, wanaume wao vile wanawake wengi wanataka.

**Com. Pastor Ayonga:** Je, mama katika hiyo nafikiri Commissioner Maranga alikuwa anataka kukuongaza kuenda upande mwingine. Upande aliotaka kukuongaza kama nilisikia vizuri, alisema badala ya kuo, hakuna kitu kingine huyo mtu aliyemdunga huyo msichana mimba angeweza kufanya ili huyu msichana afaidike na huyo mtoto aliyezaliwa afaidike? Kuliko kum-impose kwa yule mtu, kwa maana hata akimchukua anaweza kumchukua tu kama kimzigo aweke huko, hutafanya chochote. Hakuna njia ingine ungeweza kufikiria?

**Muna Mbithe:** Unajua mbeleni, mafikira yangu haikuwa ya kitu ingine lakini naona sasa iko kitu ingine mimi naelewa.

**Com. Pastor Ayonga:** Hiyo kitu ingine ni nini?

**Muna Mbithe:** Amtengee mali kiasi fulani.

**Com. Pastor Ayonga:** Sawa na kwa wale mbuzu tatu narudia swali la Doctor Maranga tena, ni kwa nini it takes so long, inaonekana kama marriage yenu hii haikuwi confirmed inaweza kuchukua muda mrefu, mbona hamuwezi kuifupisha? Ni kwa nini inangoja, hata ukapata watoto wengi na ukifa ndipo uenda kuzikwa kwingine?

**Muna Mbithe:** Wacha nikueleze kitu kimoja, unajua wanawake wanaweza kuolewa wawili.

**Com. Pastor Ayonga:** Hata watano.

**Muna Mbithe:** Na wakiolewa wawili au watano wanaweza kukaa Nairobi na wanakuja, anakuja na bwana yake na hawa watu wa nyumbani wanasema huyu ni wa Nairobi na ni wake na wanakaa pamoja, unaona hivyo? Ndio sababu ninasema, mwanamke akiolewa akimaliza miaka mbili kwa hiyo boma awe ni wa hiyo boma.

**Com. Pastor Ayonga:** Kwa mila za Kikamba ni nini mngefanya ili mufanye haya mambo, unajua makabila mengine, unaoa, ukifanyiwa harusi, mambo imekwisha. Hata siku ile ile tu, mambo imekwisha. Why does it take you people so long?

**Muna Mbithe:** Unajua Wakamba saa ingine....

**Com. Pastor Ayonga:** Hiyo ndio sijui.

**Muna Mbithe:** Wakamba wengine wako namna hii na wanakaa tu na wananyamaza na wanajua hii ni kawaida wafanye hiyo, na wanakaa tu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Nina swali mama. Je ingewezekana kupata usaidizi kama marriages zote katika Kenya zile za Kikamba

au ile ya DC, au ya makanisa zote zifanyiwe registration.

**Muna Mbithe:** Ndio.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na kama mtu ana mabibi wawili tena wote wafanyiwe registration.

**Muna Mbithe:** Ndio, kwa sababu ni wake.

**Com. Phoebe Asiyo:** Na saa zile mtu hajaoa, aeleze msichana mimi nakuoa lakini mimi pengine nitafikiri kuleta mwingine, ili huyu mwanamke ajue tu, kwamba hata naenda huu mji lakini nyingine mwingine anaweza kuja. Yaani potentially polygamous system of marriage.

**Muna Mbithe:** Hiyo ni ngumu sana, kuolewa na uambiwe iko mwingine ni ngumu sana, mwanamume anao tu akiwa amenyamaza kwa roho yake. Na kuna wengine wanaambia mabibi zao, unajua nataka kuo kwa sababu bibi yake anaweza kuwa hana mtoto, na hiyo ndio anaweza kuo kwa bibi wa pili.

**Com. Kangu:** Unajua shida yenye tuko nayo mama ni kwamba watu wetu wameenda kwa makanisa hata harusi watafanya kwa kanisa lakini nyumbani bado wanatangulia na mambo ya kinyumbani. Sasa swali inakuwa, tumefika kiwango ya kusema kuna mambo ingine ya nyumbani tunataka tuwache halafu tufuate mambo fulani ama bado tunataka kuendelea na mambo ingine.

Ndio tukisema, sheria iseme kama ni baada ya miaka miwili inaandikishwe mmeoana hata kama hizo mbuzi zimelipwa ama bado. Inaandikishwa ndio sasa kama bibi anakufa inajulikana ni bibi ya fulani, watu wako tayari kuwachana na hizi mambo zingine ama bado wanaona hii ni mila ya Wakamba lazima tufuatilie?

**Muna Mbithe:** Unajua hatuwezi kuwacha mila ya Wakamba lakini ile iko ni tuwe tukiandikisha ata hiyo mila ikiwa, tuwe tukijua hata tukiwa nyumbani mila tutafuata mila lakini nikiolewa kwa hiyo boma, nisiwekwe kama vile paka na paka wanavuta nyama, mama akifa wa aina hiyo, inakuwa....(*Incomplete*).

**Speaker:** Vita.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana tafadhali uandike jina lako pale.

**Com. Pastor Ayonga:** Machifu sasa tufanyaje?

**Muna Mbithe:** Sina shida lakini, kwa sababu ni maoni yangu.



**Com. Phoebe Asiyu:** Sasa Grace Mwanza, mama Grace Mwanza tafadhali uje hapa mbele na ufanye mapendekezo zako, naona umeandika kwa hivyo utafanya kwa kifupi tu.

**Grace Mwanza:** Majina yangu ni Grace Mwana, I am a Pastor.

**Com. Phoebe Asiyu:** Hakuna jina ya katikati.

**Grance Mwanza:** Grance Mumo Mwanza, I am a Pastor, AIC Church. Niko na mambo machache tu ya kuongea.

Kwanza ni the word of God to be given first priority in our government since it is supra culture, to our freedom of worship, preachers should be trained kwa maana kuna wengine wanainuka leo wanasema ni ma-Pastor and they are not trained. Kwa hivyo ma-Pastor wawe trained, ikiwa unataka kuhubiru uende kwa training.

Infants to be given special attention, watoto mayatima: All children to be given their rights especially the right to life because we have cases of abortions.

Biological parents to take care of their children.

Children born out of wedlock to be taken care of by both parents, ikiwa kijana amezaa alazimishwe alee yule mtoto ambaye amezaa.

To have birth rate control, watu wapewe watoto wale wanapaswa kuzaa, and myself I am suggesting that people to have a maximum of 3 children.

Drug abuse to be controlled, the government should have a way of controlling drug abuse.

The government should provide for the old women and the old men a place where they can be taken care of because we have heard cases of many of them dying for lack of care.

Freedom to choose or to marry when you are above 18, because we have problems with parents insisting the kind of spouses they want for their children. Therefore, people should be given freedom when they want to get married to choose on whom to marry.

**Com. Phoebe Asiyu:** Grace endelea.

**Grace Mwanza:** Nitafika pale.

**Com. Phoebe Asiyo:** Umefika hapa, asante sana. Kuna kitu ambacho nataka kukuuliza kuhusu pombe, nchi nyingi za dunia hazikubali kamwe kuweka advertisement kwa television au kwa radio kutangaza pombe kali, lakini ninaona hapa Kenya advertisement ya pombe kali ya shilingi kumi na tano na inasemekana kwamba inafurahisha mtu na inafanya mtu ajisikie yeye ni yeye. Sasa wewe ni Pastor na umetuambia habari ya ulevi, ungependa mambo haya ya advertisement ya pombe kali kwa TV na radio iendelee au ipunguzwe.

**Grace Mwanza:** Ningependa ipunguzwe, kama ingewezekana because we are having problems when bia imari advertised. Kwa hivyo ningependa ipunguzwe hata pia ile ina-advertise condoms ingepunguzwa.

**Com. Kangu:** Swali moja, umesema pastors ama preachers wawe-trained na ukasema freedom of worship, kuna wengine watasema kujaribu kuzuia wengine kuhubiru mambo ya Mungu kwa sababu hawana training ni kujaribu kuzuia ama ku-limit their freedom of worship. How do you reconcile those two?

**Grace Mwanza:** Okay, I would say as the other ministries like now in education cannot have a teacher who is not trained so that we call him a qualified teacher. Therefore, as other ministries we get people who are trained we can encourage so to the pastors.

**Com. Kangu:** The right to worship can be limited in certain circumstances?

**Com. Maranga:** Now, I am asking you a question Pastor, two questions. One is about the question of abortion. What is your stand on abortion? That is point number one, number two, you are also suggesting a limitation of a maximum of 3 children, is it not interfering with the freedom of choice which actually you have given? How do you reconcile the two?

**Grace Mwanza:** Abortion is killing and I have said a child should have a right to live and when you abort, you are killing. You can use other methods of contraceptives which are not killing.

**Com. Maranga:** What I am asking is, now that you are a Pastor, you know that there are some countries where abortion is legal, but I know the stand for example of the Catholic Church it is very firm, it is anti-abortion and many other people but also the medical profession who are advocating for abortion because abortion can be given on various grounds. For example, if somebody was raped and you do not want to bring forth that kind of child who was conceived under very difficult circumstances. Don't you think the land can have a right to abort at that point? That is one question I want to put to you, it is a moral question. A girl was raped, she conceived, she does not want to carry the child of the rapist and that child is innocent, what do you decide as a Pastor?

**Grace Mwanza:** The question that the government to have a way of taking care of such children because actually that child has the right to live, to allow the girl to give birth and if she does not need the child, the government to have (incomplete)

**Com. Maranga:** Pastor you did not get my point, the circumstances of that pregnancy originate from rape that was not her consent, she was raped, do you get my point?

**Com. Pastor Ayonga:** I want to come to her assistance. What Doctor Maranga wants you to say is that this girl, her mentality, her psychology, her everything is not for this child because it was done under very bad circumstances, and what you are trying to tell him is that no matter what has happened, the child who has been formed under such circumstances should be allowed to come forth and then the government picks that up and cares for that child. It will leave this woman free from caring for that child, who she would not like to see. A child can be born in a maternity ward, and the child be taken away from the mother without the mother seeing the face of that child, and it can be taken and be taken care of elsewhere. I think that is what the Pastor is trying to put across.

**Com. Maranga:** No, it does not answer my question because, why do you subject a girl to carry a pregnancy she does not want for nine months on medical grounds? She is psychologically traumatized and you want to tell me as a Pastor that you can convince that girl that continue carrying the child of a rapist? I want to put it to you, you will not do it. Thank you.

**Com. Pastor Ayonga:** Now, my other question as regards to freedom of worship. Did you tell us what that freedom of worship entails because these days people are complaining that there are so many religious bodies, others are beating the drums through out the night, and if they are in your neighbourhood, you cannot sleep. What is this freedom of worship really? And others are worshipping Satan, devil-worship. Are you saying that this freedom of worship should not be curtailed, or the freedom of worship should be whatever a person does, wherever, whatever time, whatever interference and whatever not, it should be allowed to continue like that?

**Grace Mwanza:** We should have meaning, caring for the others with knowledge of whom they are worshipping.

**Com. Pastor Ayonga:** And who should be worshiped?

**Grace Mwanza:** It is God.

**Com. Phoebe Asiyo:** There is also freedom of worship, there is a lot of devil-worship these days, you want us to give them the freedom of worshipping the devil. Okay, very good, I think you are done, thank you very much Pastor that was very good, go and sign our register. Now we want Joseph Nguvi, please be brief Joseph, wapi Joseph Ngumbi, kama hayuko tunaita

Dishon Ndonye, yuko? Kama hakuna.....

**Com. Pastor Ayonga:** Ndiye huyu.

**Com. Phoebe Asiyo:** Mzee kuja haraka, kaa hapo mbele utueleze jina lako halafu uongee juu ya mapendekezo yako kwa Katiba mpya. Unaitwa?

**Dishon Ndonye:** Majina yangu ni Dishon Dilo Ndonye. Naanzia na Wabunge, Wabunge wawe wakichaguliwa kwa miaka mitano na kabla ya kuwachaguwa Wabunge ningependelea Rais awe akichaguliwa mbele. Raisi wakati wake uwe mbele wa uchaguzi wa Wabunge, na ichukue kama miezi sita baada ya kuchagua Rais halafu Wabunge na ma-Councillor. Miezi hizo sita ikiisha, tunachagua Wabunge na ma-Councillors kama vile wanachaguliwa.

**Com. Phoebe Asiyo:** Kwanza President achaguliwe.

**Dishon Ndonye:** Achaguliwe kwanza.

**Com. Phoebe Asiyo:** Aendeshe nchi bila Bunge na bila Council. Haya, endelea.

**Dishon Ndonye:** Hapa nanasema ataendelea kwa sababu saa Wabunge wanaendelea lakini yeye anachaguliwa mbele, Wabunge wana miezi mengine ya kuendelea. Wakichaguliwa miezi sita, si wataendelea miezi zingine sita halafu muda wao uishe wachaguliwe.

Mayors wewe wakichaguliwa na watu na Chairmen wa County Councils, Chifu wawe wakichaguliwa kama vile wanachaguliwa, lakini wawe wakipewa transfer kama watumishi wale wengine.

Ningependelea watu wakiona Mbunge wao hafanyi kazi vizuri, miaka miwili wanamkataa wanachagua mwingine tena.

Akina mama wawe wakichaguliwa wakati wao, lakini napendelea kama Machakos District, pawe na mwanamke mmoja ambaye hatachaguliwa lakini yeye tunamchagua mmoja tu, kila district mwanamke mmoja achaguliwe ili awe akiwakilisha wanawake wale wengine bila kuchaguliwa pamoja na wanaume.

Urithi, naonelea hali ya urithi kwa watoto wote ni sawa lakini kunakuwa na tofauti msichana akiolewa. Akiolewa hawezi kugawiwa mali lakini asipolewa anagawiwa mali. Akigawiwa mali na apate mwanamme hiyo mali ni yake kwa sababu amechelewa sana bila kuolewa, ikaonekana huyu hataolewa.

Mali ya asili serikali inangalie sana sababu inaenda vibaya kama misitu, maji, serikali iangalie, hifadhi mali ya asili, misitu, maji.....

Elimu tunaambiwa na ya bure siku hizi lakini hakuna cha bure. Wiki moja mtoto anaenda safari tatu akiitisha pesa za kuendesha mambo ya shule, serikali iliharibu kupeana elimu ya bure, itafute pesa za kuelimisha watu wake. Ningesema ikiwezekana wanaweza kutoka Nursery mpaka wamalize elimu yao katika chuo kikuu ama vyuo vile vingine vidogo, hiyo iwe jukumu ya serikali.

Madaraka ya Rais punguzwe isiwe zaidi.

Kitu kingine ningesema ni kupindua Katiba: Ni lazima Katiba ya Kenya tuwe na referendum. Wabunge wakitaka kupindua sehemu fulani ya sheria watuuliza, sio kufanya vile wanafanya siku hizi, wakitaka kitu wanapindua leo, tunataka tuilizwe sisi wananchi.

Wale watu disabled waangaliwe sana kila kitu chao kifanywe bila kulipa kitu, kusomesha, malezi kwa disabled na wale watu ambao wamezeeka kwa sababu mtu akizeeka anakuwa taabu kwa watoto wake. Serikali iwe ikiangalia mambo ya wazee, wazee wanawake na wanaume watengewe sehemu ya kukaa.

Ningeona mshahara ya watumishi wa serikali iangaliwe ..... Wengine wanapata mshahara ya juu wengine ni chini na kisomo ni kile kile. Nafikiri nikikomea hapo ni vizuri.

**Com. Phoebe Asiyo:** Asante sana Mzee Dishon tafadhali mzee ukifika pale sasa mzee utaandika jina lako kwa register yetu na tumeshukuri sana kwa maoni mazuri. Sasa tutasikiliza Bwana Charles Maluti.

**Charles Maluti:** Nitasema kwa kifupi iwezekanavyo. Kwanza ni juu ya Presidentkuchaguliwa pamoja na bunge. Lazima uchaguzi uwe tofauti. Presidentkwanza, na baada ya kuchaguliwa kwake, tuchukue muda wa mwezi mmoja, ndio nao ma-councillor na ma-MP nao wachaguliwe. Baada ya mwezi wa pili wawe tayari na mwezi wa tatu government iendelee.

Kitu kingine ni elimu. Elimu katika Kenya imekuwa kama gorofa inawaka moto. Inaenda upande huu na huu na huu. Kwanza, tunaambiwa kuna free education in kenya, there isn't, hakuna.

**Com. Asiyo:** Pendekeza tu mapendekezo mzee.

**Speaker:** Ndio nakuja, yale mapendekezo yangu, ni free education iwe mtoto hahitajiki kuitishwa kitu chochote. Ili asome

kama wakati mimi nilikuwa nasoma sikuitishwa chochote isipokuwa kile kilihitajika cha dhati... Std. 8 wamalize hapo kila mtu awe na stand kila mtu Kenya apate elimu ya primary, sio ya kuitishwa hiki na hiki na hiki.

Kile kingine ni kuwa uchaguzi ukiwekwa hapa kama ni siku ya elections, tuhesabu kura hapa ili tuepoke ule wizi wa kura. Tukimaliza kura tuhesabu na ziende zikihesabiwa. Zisiibiwe njiani ama ziwekwe vingine.

**Com. Asiyu:** Tayari mzee hiyo sheria iko tayari. Safari hii ukienda kupiga kura zitahesabiwa pale pale, sheria ile iko.

**Speaker:** Unajua Kenya ni nchi tajiri sana na, ikiwa tajiri, ule utajiri unaweza kupatikana Kenya umechukuliwa na watu wachache sana ili yenyewe ikabaki bila chochote; kama ingechukuliwa hatua kwanza, hatungekuwa katika hali tuliyo nayo leo. Kwa hivyo, ni lazima mwenye kutumia mali ovyo katika Kenya afikishwe kotini, afungwe, alipe na vitu vyake viuzwe vile amechukua kwa magendo. Ndivyo mali irudishwe kwa wananchi. Katika Kenya yote, iko na rasilimali ya nchi nyingi lakini haitumiwi ili kutoa mapato kama tunajua Kenya yetu ni agricultural. Kuna maji kama hii mvua imenyeshwa hapa, maji hii yote imerudi kwa bahari. Na nchi hii na nchi zingine huwa na ukame. Hayo maji yangeshikwa tayari hatungeendelea kupata njaa. Yanyunyishiwe katika kila mahali kwenye ukame tupate chakula na tupate wafanyi kazi kwa sababu iko mahali ya kufanya kazi kutoa mazao.

Kile kingine, katika Kenyakuko na ukoloni mamboleo, kama tuna factory na wenye kushikilia hii factory wametuweka kama stairs. Unakuta mtu anaandikwa wiki tatu anafutwa, asitimize ile miezi mitatu ya kuandikwa. Anawekwa mwingine, na ile mshahara anapewa hawezi kujimudu hata kidogo. Kama sasa ukimpa mtu shilingi mia moja atoke hapa. chakula hali, ana watoto nyumbani ana bibi, ile mia moja, itamfaa nini? Pendekezo, watu wengi wameshikilia hii kitu ni wahindi, wawekewe sheria ya kuandika watu sawa sawa na wawape mshahara tosha. Sio ile mshahara wanawapa watu mia moja, mia mbili, mia na hamsini. Na wahakikishiwe ya kwamba mtu awe kama kibarua kama ni miezi tatu na aandikwe permanent. Hawa wametunyonya hata kupe ni afadhali. Na mimi namalizia hapo.

**Com. Asiyu:** Asante sana Mzee John, tumeshukuru sana kwa maoni yako, tafadhali kama ungefika pale uweke jina lako kwa register yetu itakuwa mzuri. Na maoni yako tumeyachukua. Sasa tuko na councillor John Kimili, kama uko hebu fika hapa mbele, na utafuatwa na bwana Ndunda S.M ukishamaliza maoni yako mzee councillor.

**Clr: Kimili:** Madam chairlady na commissioners wengine, jina langu ni John Kimili. Mimi ninawakilisha wodi ya kalama location constituency ya Machakos. Ningependekeza political parties ziwe less than ten, na ziwe zinajitafutia uwezo wa kujiendesha.

Pia ningependekeza any ruling party iwe linked kutoka kwa Central Government. ningependekeza mayors na wenye viti wa Local Authorities waendeleo kuchaguliwa na madiwani wenyewe. Sababu yake wananchi wa kila mahali hakuna njia wanaweza

kujua mwenyekiti tuseme tukiwa Machakos na tuseme mwenyekiti anatoka kama Kangundo hapa hatuwezi kujua. Lakini wale madiwani wanaokaa na yeye pale, wanamjua na wanaona vile anafanya kazi. Kwa hivyo ningependekeza huo mtindo uendelee hivyo hivyo.

Elections ningetaka ziendelee pamoja, election ya madiwani, ya wabunge na ya rais. Iendelee kwa wakati mmoja. Kwa sababu tusipofanya hivyo kama tuna mjumbe hapa na hanitaki niwe Diwani, akiwa free anaweza kuingilia ule uchaguzi na usiwe fair kwa wananchi. Kwa hivyo anaweza kusukuma yule councillor ama yule Diwani anayetaka yeye mwenyewe na isiwe ndio mapendekezo ya wananchi. Kwa hivyo ningetaka ziendelee pamoja zote. Ndio kila mtu awe busy na asiwe na wakati wa kuangalia mambo ya mwingine.

Ningependekeza pia Katiba kila wakati iwe ikiangaliwa na wabunge, kwa sababu tuliwachagua kama wabunge wetu na tunawaamini na tunachagua yule tunafikiria he is the best for our area. Kwa sababu kama hana hiyo wajibu pengine they have no business of being there. Tumewachagua kutengeneza sheria. Kwa hivyo ningependelea waendelee kuwa na uwezo wa kubadilisha Katiba for time to time kama wajibu wao.

Property ownership, ningetaka kuwe na uhuru wa kila mtu yeyote awe mwanamume mwanamke awe na uhuru wa ku-own property kwa mahali popote katika jamhuri yetu. Ningetaka lugha ya taifa idhaminiwe. Wakenya wote waweze kuungana kwa kuwa tunaelewana. Lakini mimi nikiwa naelewa na Kikamba na mwingine haelewi naweza kumsengenya wakati wowote na nimbandike kitu fulani, pengine kiende kombo.

Provincial administration ningetaka ikae, lakini this must be chiefs wachaguliwe na wananchi wa ile eneo ambayo wanatoka ndio wawe wanajua wana wajibu wa kutumikia hao wananchi vizuri, wasiwe kama kings katika ile area. Ikiwa na kosa na imejulikana kwa Serikali wawe wakiadhibiwa hapo hapo na ikiwa kuna chief ambaye ame-prove kuwa capable kuwa promoted, na ana qualifications zile zinatakikana, anaweza kuwa promoted as the D.O.

Kuna wale wazee wengine wa vijiji ambao wanasaidia administration na hawa ni wa muhimu sana kwa sababu ile kazi wanafanya hata saa ingine wanafanya kazi zaidi ya assistant chief, kwa hivyo ningependelea Katiba iwaruhusu hawa wawe wakipewa kitu, kama sivyo waondolewe kabisa.

Ningetaka kuwe na free education kutoka darasa la kwanza mpaka la nane, na iwe ni lazima kwa kila mtoto. Kwa sababu hiyo ni njia moja ya kupatia watoto haki yao. Na ikiwa ni free education, tusiwe tukiona watoto wanatumwa na waalimu kila wakati, 'nenda mkalete hiki, nenda mkalete kile'. System yenyewe ifanye mpango, iwe mtoto akienda shule, kazi yake ni kusoma mpaka wakati ule anamaliza shule aende nyumbani.

Uchaguzi - kama mtu yeyote anasimama anataka kitu fulani kama ni diwani, kama ni mjumbe, tuwe equal. Awe ni mwanamume

ama ni mwanamke bora auze lugha yake kwa wananchi wale wana kura. Kwa sababu hii mambo ya kusema kama ni wanawake wawekewe a special consideration, saa ingine itatulazimisha tuweke mtu ambaye ni kiwete na hajiwezi kwa ku-deliver goods kwa wananchi.

Pia, medical scheme ama mambo ya matibabu yawe free kwa kila mwananchi. Kwa sababu kama siku hizi tunaangalia watu wengi wanakufa kwa sababu hawezi ku-afford medical services. Na sisi wote ni kama tumekuwa wagonjwa. Kila mtu akionekana ni mgonjwa ama akifariki tunasema ni AIDS, ni ugonjwa pengine wa kawaida na mtu hawezi ku-afford na tunampoteza.

Discipline ya watoto shule, naona hiyo ni ya lazima. Kwa sababu hata nyumbani wazazi wengine tumezoea. Mtoto akinikosea namwambia nitaenda kumwambia mwalimu. Bora mwalimu ajue ni kiasi fulani ya punishment anapatia mtoto, asiwe excessive, ikiwa excessive pengine iwe na disciplinary committee ama board fulani ya kuangalia mwalimu ameenda excessively na anaweza kuwa disciplined hata na yeye kwa hiki na kile.

Pia, ningependekeza Kenya kama agricultural country, kuna nchi kubwa ambayo inaonekana inakaa bure na watu wanaendelea na njaa, Tunaendelea kuomba misaada ya chakula hapa na pale, tumekaa kama beggars. Ningependekeza sheria ama Serikali ifanye mpango kuwe na watu wale ambao ni landless na pengine wamemaliza darasa la form four na kuendelea juu. Wawe wakikatiwa sehemu fulani watafute pesa zao pale daily living na hata kulisha watoto wao.

Ningependekeza Local Authority iwe na uwezo wa kupitisha mambo yao bila kuomba omba kwa Serikali kuu. Kwa sababu councilors wengine wanaenda wanakuta wana shida and their hands are tied hawawezi kufanya chochote. Kwa sababu the executive or the senior officers of the council ni wafanyikazi wa Central Government, and they cannot discipline them. Ile system inafuatwa ni ndefu sana na kwa hivyo, chief officers wanaendelea kufanya kazi vile wanataka hata ikiwa ni mbaya. Kwa hivyo ningetaka councilors wawe na uwezo wa ku-run their own council kulingana na mahitaji yao.

Mfanyi kazi yeyote awe ni wa Serikali ama ni wa private sector, wakati ukifikia wa kwenda retire, atayarishwe na mambo yake, pesa na nini, aende kufurahia matunda yake. Kwa sababu ameyafanyia kazi kwa muda mrefu, amechoka, amejinyima, na ule mtindo wa kuwa anafuata pesa zako ukiwa umetoka kazini, na huna pesa zimewachwa huku, that opens room for corruption. Kama huku utaenda uambiwe kama unataka tumalize hii leo fanya hivi. Hizo ni pesa wanapeana. Kama ni wakati unatupa, na pengine umetoka mbali na huna uwezo wa kuja hapo kesho.

Ningetaka kuwe na tume mbili za kuchunguza mishahara ama marupurupu ya wafanyi kazi wa Serikali, na ingine ya private sector ili kila tume iwe inapendekeza ama inafikisha mambo ya wafanyi kazi wa that sector kulingana na vile wanaona mambo yanaendelea, vile wanaona gharama ya maisha inaendelea na hivyo hivyo.



Isiwe kama juzi tulisikia wajumbe walijiongezea pesa chungu nzima na madiwani wangali wanalia lia ofisini na wao ndio wanakaa na wale wananchi ambao waliwachagua wajumbe. Na sisi ma-councillors ndio tuko karibu na wananchi, mwananchi akiwa na shida ya school fees ama ya ugonjwa ama ya njaa anakuja kwa councillor kila asubuhi, na councillor hana uwezo, ile pesa anapewa pale ni kidogo sana, na wajumbe wana-enjoy. Ana pesa zile pesa na hata mwezi mzima hawezi kuonekana kwa electoral area yake. Kwa hivyo ningependekeza kuwe na tume ambayo inachunguza mambo ya madiwani.

Freedom of worship iwe controlled to an extent kwa sababu ule mtindo wa kusema kuna uhuru wa kuabudu siku hizi umeonekana ni kama wengine sio kuabudu, ni kazi wanafanya for their living. They have not even gone for any course or training, they are not even registered in the government, lakini kwa vile tunasema kuna freedom of worship, kila mtu anasimama kwa soko, pengine kuna dispensary hapo karibu kuna ugonjwa wanatibiwa hapa na anawapigia kelele. Kwa hivyo ningetaka kama ikiwezekana, hivi leo tungesema Katiba iseme no more registration of churches or religions ama nini, zile ziko kama sitosheki hapa niende kwa hiyo ingine lakini not new denominations.

Ningetaka kupendekeza pia ugawaji wa national resources. Mali kama ni ya Serikali iwe inagawiwa kila sehemu kulingana na population. lakini sio kuwa kwa vile hiyo ni region kama ingine kama ni province, iendelee kulingana na population kama sisi sote ni wananchi wa Kenya, inafaa tutumikiwe the same.

Mambo ya wasichana kama ni my daughter na ameolewa mahali, ningetaka akae na adabu kwa ile boma na atafute mali yake akiwa hapo. Lakini hii mambo ya kusema aje hapa kwangu akatiwe sehemu, kuna hata wanaume wengine wana mtindo wa kumwambia bibi nataka tutafute mali kwa hivyo nenda kwenu ujifanye umerudi ndio nikija kule tugawiwe kitu. Kwa hivyo ningetaka mwanamke akiolewa akae na adabu na atafute mali yake kule lakini sio anakuja kuchukua sehemu hapa. Sababu hiyo itaendelea kuongeza watu kuacha mabwana zao na itaongeza ile shida ya ukimwi. Na ni hayo mwenye kiti, ningetaka kukomea hapo, asante.

**Com. Asiyu:** Asante sana councillor, sijui kama kuna swali yoyote kutoka kwa wenzangu hapa.

**Com. Kangu:** Na bwana councillor, hii mambo ya freedom of worship, umesema wengine wamegeuza imekuwa kama biashara. What is the best way of controlling this? Kwa sababu kama unasema ni biashara na ni kweli those make a lot of money, wengine wana-run businesses, they run hospitals, they run schools from which they make money. Do we subject them to income tax ama tufanye namna gani?

**Cllr. Kimili:** They should, kwa sababu hiyo ni income wanapata, there is no way they should be left to go without saying anything like any other employee or any other person. And out of that living anakata sehemu inaenda kwa Serikali kama tax.

Kwa hivyo huyu naye kwa vile anapata income kutoka pale na wengine tumeona wamekuwa very rich hata kushinda wale tunafanya kazi. Kwa hivyo ningetaka wawe subjected to income tax kama wananchi wengine.

**Com. Asiyu:** Niko na swali moja hata mimi. Umesema kwamba chama kinachotawala kiwekwe mbali kabisa na Central Government, na je, kama hii chama ndicho kimechagua ma-ministers, maana ndio imeshinda uchaguzi, na pia ndio imeteua ma-permanent secretaries na wale wote wanaofanya kwa Central Government. Ni nani sasa atalinda watu wa Central Government kama sio wale watu waliochaguliwa na ile party iliyoshinda?

**Clr. Kimili:** Kama ni financial matters, chama kisiwe kinatumia pesa za Serikali.

**Com. Maranga:** I want to ask you something, umesema unataka Local Authorities iwe autonomous imetoka kwa Central Government. Ungefikiria Local Authorities wangukuwa wanafanya nini kama wangepewa huo uhuru wa kujiamulia maneno yao?

**Clr. Kimili:** Ni uwezo tu wa kupitisha maneno yao, kama ni senior officers wa council kwa sababu amejiriwa na Central Government and the Local Council cannot discipline him kama amekosa. Anataka kufanya kazi vile anataka, na hawa ni madiwani wamechaguliwa wamechaguliwa, na watu wanaendelea kulia.

**Com. Asiyu:** Nataka kukuambia hiyo halafu nitampa pastor Ayonga nafasi. Councillor wewe ungetusaidia sana kwa mambo ya Katiba mpya. Sasa wewe unaongea tu mambo ya wafanyi kazi wa County Councils na Municipality. Lakini hujatuambia ile kazi ambayo Local Authorities wanaweza kufanya. Zamani ndio walikuwa wanatengeneza njia, ndio walikuwa wanaangalia mambo ya shule, mambo ya ma-dispensary na kadhalika. Sasa wewe ukiongea tu juu ya wafanyi kazi na unawacha umuhimu wa kazi ya Local Authorities, tutajua namna gani vile unataka kazi ya Local Authorities zitengwe?

**Clr. Kimili:** Madam Chair please, ni hiyo shida, hawa senior officers wanakuwa vikwazo. The councilors don't have powers kusema twende tukate barabara mahali fulani na pengine kuna pesa, huyu amekaa kama kikwazo, senior officer, na council kazi yake ni kupeleka huduma kwa wananchi.

**Com. Ayonga:** Com. Asiyu amekuuliza swali na ambalo ningekuuliza na sikutosheka na jibu, kwa maana kila wakati unasema kwamba wale senior officers ndio wamekuwa mzigo kwa Local Government. Ni kama kwamba kama hao watu wangetoka, mambo yote yangukuwa sawasawa na hali ninasikia na wewe unasoma pia kwa magazeti, bankruptcy ambayo imejaa katika local councils zetu, na services ambazo haziwezi kuwa rendered na hali watu wanalipa rates for this and rates for that, mara hakuna maji, mara hakuna taa, mara barabara hata within, katika councils zetu. Senior officers ndio wamefanya haya mambo yote? Na tena councils hizo zikipewa nguvu watazatumia namna gani? kwa maana mtu akiwa mwaminifu kwa kilicho kidogo huyu atakuwa mwaminifu kwa vilivyo vingi, au sivyo? Sasa hapo hujatuweka vizuri.

**Cllr. Kimili:** Nimesema kile kinafanyika councilors wanaona kuna haja ya kupeleka hiyo huduma mahali fulani within the area as the council area of jurisdiction, lakini officer amekuwa hataki.

**Com. Ayonga:** Na pesa ziko?

**Cllr. Kimili:** Pesa ziko kwa sababu he is the signatory of everything.

**Com. Asiyo:** Na hizo pesa zinatoka wapi?

**Cllr. Kimili:** Inatoka from the Local Authority na inaongezwa na zinazotoka kwa Central Government, lakini ikija hapa... inatosha.

**Com. Asiyo:** kufanya kazi gani?

**Cllr. Kimili:** Kazi za huduma kama ni barabara...

**Com. Asiyo:** Mna pesa za kutosha za kutengeza barabara kwa County Council?

**Cllr. Kimili:** Ikiwa well-managed.

**Com. Asiyo:** Na mahospitali?

**Cllr. Kimili:** Pengine inaweza kuangaliwa.

**Com. Asiyo:** Okey, tumeshukuru bwana cllr. Kimili, sasa ni bwana Ndunda S.M tafadhali kuja na uchukue nafasi. Is it D.M or S.M?

**Mr. Mutua:** Samson Mutua Ndunda.

**Com. Asiyo:** Bwana Ndunda tafadhali endelea kutoa habari yako lakini kwanza taja jina lako mashini ishike ndio uendelee kuongea.

**Mr. Mutua:** Naitwa Samson Mutua Ndunda. Nina maneno matatu hivi ya kuzungumza. Ya kwanza ni kuchaguliwa kwa rais. Kulingana na experience ambayo imekuwa hapa na mahali pengine, Presidentni lazima awe na minimum education na hiyo

minimum education should be form four and above. Sababu yake, ikiwa hana education enough, ataweza ku-sign ama kutia sahihi kitu ambaye hafahamu zaidi.

**Com. Asiyo:** Na hiyo umetueza vizuri.

**Mr. Mutua:** Na hiyo kwa sababu akiwa hana elimu ni makosa. Jambo lingine ni juu ya wale ambao hawafanyi kazi na Serikali ambao walistaafu. Walikuwa wanafanya kazi vizuri na wakishatoka wanakuwa kama mchanga tu. Serikali haiwatunzi vizuri. Ikiwa mishahara umeongezewa kwa sababu ya mambo mengi hawashughuliki. na ukiuliza watasema nitafanya hivyo wakati pesa zitapatikana, lakini hazitapatikana.

Ingingine ni kuchelewa kwa mishahara yao. Hao watu wengine walikuwa na watoto wachanga, hawana fees na kwa hivyo ikiwa analipwa tarehe kumi na tano, ama kuendelea, unaona ukiulizwa ‘mzee ulikuwa unafanya nini, wapi, ulikuwa huku Nairobi’ unaambiwa na wale watu ambao unaketi nao yuko nyumbani hapa anataka kutengeneza mambo yake lakini haitawezekana. Napendekeza wawe wakilipwa kama mwisho wa mwezi.

Kitu kingine, ni medical care. Hawa watu ambao wanafanya kwa Serikali ni watu ambao wanahitaji msaada kwa sababu hospitali bei inaenda juu kwa hivyo mtu akiwa mgonjwa atakufia hapo tu kwa sababu hana pesa ya kulipa. Kwa hivyo ningependekeza kuwe na package. Ile pesa ambayo Serikali inaweza kuwalipia wawe wakiletewa kama wale wafanyi kazi wengine wa Serikali.

**Com. Asiyo:** Yaani wafanyi kazi walioajiriwa pekee yake watibiwe na wananchi wengine waache kwao?

**Mr. Mutua:** Hapana nasema, kama wananchi wengine ambao wanafanya kazi kwa sababu ukiwa civil servant sasa. Kuna allowance ya medical kwa hivyo hiyo nataka iwe ikija kwa wale ambao wamestaafu.

Jambo la mwisho, ni development. Ningependekeza kwa kila district, nafikiri iko karibu sabini, kuwe na a plant. Serikali iangalie mahali hapo ni kitu gani tunaweza kuifanyia katika hiyo district ili watu wale tupunguze umaskini.

**Com. Ayonga:** Lakini si ni wewe ungetuambia Serikali ifanye hivi na hivi ili ipunguze umaskini?

**Mr. Mutua:** Okey, kwa kupunguza umaskini kila district iwe na factory ama a plant, kila district. Asante.

**Com. Asiyo:** Kabla hujaenda kuandika jina lako kwa register yetu pale bwana Ndunda nataka kujua kama kuna commissioner ana swali yoyote. Okey, hakuna swali kwa hivyo unaweza kuenda pale kuandika. Ninashangaa unahusika juu ya mambo ya afya ya watu wa Kenya na hujasema wapatiwe free medical care. Unataka tu wawe retirees ndio watibiwe. Lakini umesema...

nenda pale tu uandike jina lako na basi ...Sasa tuko na Rosemary Makau, tafadhali kuja hapa mbele uongee mama kwanza uanze na jina lako ili ishikwe kwa jambo hili kwa hii kimashini na naona kwamba kama umeandika mambo yako kwa karatasi, kwa hivyo utaongea tu mambo ya muhimu hapa na pale halafu utupatie memorandum tutaweka kwa computer yetu kule Nairobi. Asante.

**Mrs. Makau:** Kwa jina naitwa Rosemary Mbithe Makau, mimi ni member wa 3Cs katika division yetu ya Kalama. Nitaongea mambo machache nikianza na political parties.

Kwa maoni yangu mimi, naonelea vile vyama nyingi sana hapa Kenya vinaundwa. Naona ni vizuri kuwe na taratibu ama mpango wa vyama vile vinaweza kuanzia, maana zikiwa nyingi sana vinaongeza shida. Watu wengi wanaanza kugombana, kuchukiana, pia inaleta confusion kwa watu wale ambao wanataka tuwachague.

Ile ingine kwa maoni yangu mimi naona kama kungekuwa na limitation ya hivi vyama, viwe kama viwili hivi, ili chama kimoja kikitawala kile kingine kiwe kinaweza kusaidia kwa upande wa upinzani badala ya kuwa na hivi vyama vingi sana. Kama kuna vyama pengine wanapendelea kuwa na vingi, pengine viwe vinahusika kwa upande wa maendeleo sio wakimaliza elections wanapotelea ama wanaanza vita. Wawe wanaweza kuchangia maendeleo katika nchi yetu.

Kwa upande wa elections, mimi naona wakati mwingi tukiwachagua wabunge, wengine huenda katika bunge na wanapotea kabisa kutoka kwa watu wale waliowachagua. Na wakati walikuwa wanaomba kura walikuwa wametua giza mambo mengi sana. Lakini sasa wakiingia katika bunge, kama wanaona kuna shida fulani, ama mambo mengine walioyotuahidi hayawezekani, nafikiri ni vizuri warudi kwetu tuje tufikirie pamoja tuone ni vipi tutafanya ndio tuweze kuendeleza yale mambo ama tuone tufanye vipi badala ya kupotea. Wengine wanaanza kuuliza yule mtu tulichagua ameenda wapi hatumwoni.

Pia naona kwa upande wa kumchagua president, kwa maoni yangu President sio vizuri akiwa ni MP wa mahali fulani kwa maana President ni wa nchi yote, wa state na ni wetu sisi sot. Maana akiwa ni MP wa mahali fulani na ana uwezo mkubwa kuliko wale MP wengine anakaa nao hapo. Kutakuwa na shida maana ana uwezo mkubwa kuliko hao. Kwa hivyo naonelea wakati wa kuchagua. tumchague MP halafu watu wote katika nchi sasa wachangie kwa kumchagua president. Lakini kama ametoka kwa MP mmoja akiwa President kuchaguliwe MP mwingine pahali yule alitoka.

Kwa wakati wa wataka kura wanaomba kura kutoka kwa wananchi, mimi naona ni vizuri kuwe na mpango ndio wawe na tabia nzuri, kwa maana mara nyingi inashinda watu kama wanawake watu wasiojiweza, vijana kupambana na wao. Na kwa sababu ile lugha wanatumia pengine kwa mwanamke mwenye tabia mwenye anajiheshimu sasa akisimama hapo waanze kurushiana maneno yale machafu na wale watu, watoto wake wanasikiliza, bwana yake anasikiliza, majirani wanasikiliza, wanawake hawawezi hiyo ni ngumu sana kwao ndio wanaanza kurudi nyuma kidogo unaona hawapendelei sana kujitokeza.

Pia, kama ni mtu kijana na anataka sana kuingia kupambana na wao katika kura, akiingia hapo anaanza kuitwa kijana, mtoto, wewe tunakujua hivi na vile na vile, sasa anaona haya na hata kurudi nyuma. Kwa hivyo kuwe na restriction, kuwe na discipline ndio watumie lugha nzuri, wananchi wanawaelewa wanaweza kujua ni nani mzuri hata asipotukanwa.

Nikija upande wa basic rights, nikiangalia vizuri, nchi yetu haizingatii sana mambo ya basic rights kwa watu wake. Maana tukiangalia upande kama maji masafi hata ya kutumia. Health care, education na mapato hata chakula. Tunaona watu, kuko na difference kubwa sana. Kuna watu wengine wanataabika sana kama sio wa nchi hii na kuna wengine wametosheleka kabisa. Kungekuwa na a little balancing na ninaona Serikali ingejaribu sana tuweze kuwa na maji ya kutosha maana maji ni uhai. Na watu wakikosa maji, ni lazima wawe na shida nyingi.

Pia, wakati mvua inaponyesha hii maji yote inapita inaenda mbali sana na tunaachwa na ule ukame wetu. Tungekuwa na technology ya kuzuia hii maji yote isipeleke mchanga wetu wenye rotuba kupelekwa mbali maana mchanga ndio mali yetu. Serikali ikiwa na mpango mzuri wa hiyo technology tungefaidika sana wananchi wa Kenya Ule mpango mwingine ni ule wa health care. Kwa kweli Serikali yetu imetuahidia kuwa na matibabu ya bure, lakini tukiangalia sio kweli maana tunaona vile watu wanataabika sana. Mara yote dawa ni kununua hata ile health center iko karibu ukienda unapewa kibarua unaambiwa nenda ununue hii dawa haiko ama unanunua hapo papo.

Sasa hiyo inakuwa ni shida kubwa na watu wengi wale wasio na mapato mazuri wanaumia tu wakiwa ndani ya nyumba.

Upande wa mapato nasema, employment ningeweza kuwa na nafasi zitafutwe lakini nasema watu wapatiwe ujuzi mzuri waweze kutumia the available resources in our country, so that we can earn from there those who are not employed.

Na Serikali iangalie ama the government should have the responsibility of ensuring that Kenyans enjoys the basic rights. All Kenyans enjoy their basic rights. Even the unborn children so abortion should be strictly illegal. Mtu mkenya kama mtoto niko na mimba ndani yangu na mimi ni mkenya, yule mtoto pia hata akiwa hajazaliwa ni mtu wa Kenya na ni vizuri apewe nafasi ya kuja kufurahia kama vile nimefurahia nchi yangu. Nikiwa siko huku yeye ataachwa na ndiye na atakuwa kenyan. Kwa hivyo naona Serikali hapo iangalie sana mambo hayo.

Na kuna ile haki ama haki za wanawake ningezichangia kidogo hapo, the interests of women are not fully guaranteed in the constitution. Women legally married should have the right of ownership of the family property. For that, if my husband dies nobody will claim or come to complain about our land. Na kama bwana ameo wanawake wawili, na ifikie wakati mmoja afe, tuseme kwa mfano kwa mila yetu ya Kikamba bwana anaweza kuwa na wanawake wawili na awe ameo amepelika ile mahari inatakikana wote ni watke lakini incase of death, azikwe kwa bibi yake wa kwanza. Kusiwe na kujadiliana ni wapi na ni wapi. Na kama bwana ameandika kitu ameacha nyuma ndio ile inaitwa will, ifunguliwe wazi kwa watu wanaohusika wote waione wajue amesema nini. Mtu mmoja asiseme ni mimi mke wake ama ni mimi mtoto wake na nimeiweka. Ifunguliwe wote waweze

kuona amesema nini.

Tuseme kama kuna mwanamke ambaye ameolewa na mtu na wamekaa. Sisemi kuoia maana walikuwa wanakaa tu. Kama wamekaa muda wakiwa pamoja na haijafahamika kama ni ndoa ama wanakaa sasa huyu mwanamke wakati mwingi tunaona kunatokea shida wengine wanaanza bwana anatoa mahari mwanamke akiwa ndani ya sanduku apeeane huko ndio akubaliwe azike. Hiyo shida isitokee kama mwanamume amekaa na mke kwa muda wa miezi sita wakiwa pamoja kama bibi yake kwa ile hali ya ndoa. Ni lazima amuoie, maana sasa amemharibia ile heshima yake na akiwa na mwanamke mwingine basi na huyu mwanamke awe amepata watoto, huyu mwanamume awe responsible alie wale watoto mpaka waweze kujitegemea.

Incase of the disabled, they should be given equal chances to participate as candidates in elections. Wapatiwe nafasi nzuri kama kuna wanaweza kuingia kwa siasa ama kwa elections na wakati mwingine tunaona kuna shida katika mijengo yetu ya Kenya kwa wale wasiojiweza wanakuwa na shida sana. Tujaribu kuwa na mijengo mizuri ambapo kama ni office na ni mtu asiyejiweza anafanya kazi hapo, anaweza kuingia kwa urahisi na kutoka kwa urahisi. Namalizia hapo.

**Com. Asiyu:** Mama asante sana kwa maoni yako. Kwa maana umeandika tafadhali peana hiyo karatasi pale na uandike jina lako. Sijui kama pana swali.

**Com. Kangu:** Mama umesema vyama, vya siasa vipunguzwe vibaki viwili kwa sasa tuko nayo zaidi ya arubaini. Tukiamua ibaki mbili tutatumia utaratibu gani kusema hii ndio itabaki na hii ndio itatolewa?

**Mrs. Makau:** Ndio maoni hapo mwanzo nikasema kungekuwa katika nchi yetu ama Serikali yetu ingekuwa, hata kama haiko sasa, lakini ndio maana tunaandika Katiba siku ya leo. Kungekuwa na taratibu ama mpango wa kufuata chama kijiandikisha ndio wasije wengi kujiandikisha kwa vyama vingi.

**Com. Ayonga:** Mama ulisema ingekuwa kitu kizuri kama bwana anafariki azikwe kule kwa bibi yake mkubwa. Bibi wa kwanza. Je mila ya Kikamba inasemaje?

**Mrs. Makau:** Mila ya Kikamba inasema hivyo.

**Com. Ayonga:** Kwa hivyo shida imetoka wapi?

**Mrs. Makau:** Imetoka sasa siku hizi wake wengine wakiolewa pengine bwana ameenda mahali pengine na anakaa mahali pengine tunasikia wanaanza kuvurutana, yule anataka apelekwe kwake, na huyu mwingine anataka apelekwe kwake. Pengine wale wako siku hizi ni wale wajane ..

**Com. Asiyu:** Asante mama, umefanya vizuri miaka hamsini ijayo hiyo maoni yako itakuwa mzuri kwa maana sasa bado kuna culture lakini itakuja potea. Sasa ningependa kuuliza bwana Wilson Mativo, yeye ni councillor. Mzee amekuwa na sisi hapa karibu kwa muda mrefu, unajua maoni yako yatakuwa ni ya maana na pia utayasema kwa kifupi na kinaganaga ili watu wafahamu ile Kiswahilisanifu au Kizungu vile utakavyopenda.

**Mr. Mativo:** Asante sana, madam chair. Jina langu ni Wilson Mativo Kyalo, councillor kutoka Koola location, vice chairman Masaku County Council. Na ningeanza kusema ya kwamba ningepomba Katiba yetu ianze na kusema sisi waKenyatunasema hivi, ikiwa tunataka Katiba ibadilishwe ipate theluthi moja ya waliopiga kura. 1/3 of those who voted.

Pili, nataka hii Katiba iandikwe na lugha, Kizungu, Kiswahilimpaka Kikamba. Iandikwe iwe nikiwa shambani ninaweza kusema wakati umefika wa kuchagua rais.

Ningeruka kwanza nizugumze mambo ya shamba. Nataka tuwe katika Katiba, tuwe na permanent land commission. Hii permanent Land Commission iwe ndio inachunguza mambo ya misitu, mambo ya government land, mambo ya mineral resources, mambo ya kuendesha ni wapi ambapo tunaweza kupata minerals exploitation na pia iwe na uwezo wa kukaa chini na kujua kwamba wewe ulinyakua shamba letu ukajitayarisha tuinyakue hiyo shamba kama ulikuwa wakati ulipokuwa President au wakati ulipokuwa member of parliament, ama wakati ulipokuwa na nguvu fulani. Land Commission ambayo haitaingiliwa, iwe inaweza kusema haya. That is what I will say is corrupt means contrary to the government interest.

Kusiwe na mtu yeyote ambaye anaweza kuwa na zaidi ya acre mia moja. Wengine wana 24,000, wengine wana kila kitu. Mambo ya nyumba sitazungumza, wewe kuwa na nyumba Nairobi, kuwa na nyumba Mombasa na nini lakini tukiingia katika land mwananchi hapa anatembea bila land ya robo acre na wewe una 24,000. Ulizaliwa namna gani? itakuwa ina-receive and assist government application of compulsory acquisition of private land to simplify all land-locks in the government, ile permanent commission iwe mimi mwananchi nikiwa pale, nikisema namna hii ninaweza kusoma ile land law nijue inasema namna gani.

Mahali ambapo patatokea ubishi tunatatizika ningependa ile Permanent Commission iwe na branch mpaka chini. Iwe imepeana uwezo mpaka chini, na pengine hapa tuna shida ya mipaka. Tunang'ang'ania kichaka. Kuwe kuna wazee wamechukuliwa kutoka ukoo ule na wazee kuja kusikiza hii dispute katika jambo la Mativo Kyalo ambao sio ukoo wangu. Ukoo wangu siusikilizi. Ukoo ule utolewe wazee waje wasikilize.

Ile ingine inheritance imezungumzwa sana, niko pamoja na wale waliosema wasichana wale ambao hawajaolewa wapewe nafasi ya kupewa mali kwa kiwango fulani.

Uchaguzi wa president.... ama kwanza niseme uchaguzi, 1963 tulichagua councilors siku yao, Members of Parliament siku yao



na Prime Minister. Au President siku yake, lakini ilikuja ikaonekana wewe mpaka Councillor ukitaka kuchaguliwa mpaka uimbe mjumbe kwa kuwa unaanza kuchukuliwa kwanza na bila kumwimba yule mjumbe huwezi kuchaguliwa. Kwa hivyo ningali ninaona ile tunaendelea nayo, uchaguzi uwe hivyo hivyo na ukiwa hivyo hivyo President asiwe anatoka constituency fulani. Achaguliwe bila ya kutoka constituency yoyote.

Pia, awe na running vice president. Hapo President awe na two terms, maximum of five years each. Parliament iwe na uwezo wa kumshtaki President ikiwa anakosa ameifanyia nchi lakini ipitishwe na 75% ya members of parliament.

Prime Minister awe appointed na President lakini wakati wa kutaka kumtoa asiwe na uwezo wa kumtoa atolewe na bunge 50%. Ninakataa kata kata majimbo. Majimbo yataleta ugawanyiko mwingi zaidi katika nchi hii na watu wengine maanake tumehamia kama sisi Wakamba tuko Shimba Hills, tuko Mariakani, tuko Mwea, tuko Taveta. Ikiwa ni jimbo utaambiwa usiseme, fuata wale wenyeji wanaosema hawa. Itakuwa ni kuwindana na ni kama watu wanataka pengine hawana freedom vile tunataka. Kwa hivyo mambo ya majimbo yataleta mvurugano. Tukae Taveta na wajaluo, na wakikuyu, waende settlement Tana River na sisi tukutane Mwea na wameru na waambu tuwe sawasawa, mahali popote tunakaa kusiwe kukawa kuna mmoja mkubwa kuliko mwingine.

Nataka kuja juu ya Local Government. Local Government ziwe na autonomy ile ilizungumzwa na mwenzangu councillor hapa. Zikiwa na autonomy, wachague chairman na vice chairman wachaguliwe na raia na wakienda wale madiwani wachague speaker na wao watapanga budget yao na resources zao itakuwa namna gani na ili Serikali kuu iwe ingali iko na nguvu zaidi 25% ambayo inayotoka kwa Local Government iende kwa Central Government. Any collection from the Local Government iende 25% to the Central Government na wao walipe madiwani itoke katika consolidated bank mshahara wa madiwani utoke katika Consolidated Fund na walipwe not less than 70, 000 per month.

Kiwango cha elimu cha madiwani wawe form four or equivalent maanake elimu ndogo ndogo saa ingine itaharibu mambo. Na kule Turkana walisema maana watu wa form four shauri yao. Hiyo mtaangalia lakini nimesema equivalent.

Human rights- to investigate should be a Human Rights Commission ambayo itakuwa ina-investigate any breach of fundamental rights. To examine the causes of economic and social disparity and conflict among the people of Kenya then to educate them.

Katika vyama vya siasa, kisiruhusiwe ki-apply lakini kiwe na one million members. Not less than registered members than one million for one to be registered as a political party in Kenya. Wafungwa wale wanaofungwa katika majela, ikiwa mtu amepatikana na haya makosa madogo madogo ya six months ya kuiba kuku, afungwe six months aje kulima huku kwetu barabara. Ya nini wawekwe wote jela zimejaa mpaka wanakufa huku jela?

Ya mwisho, civic education, hii ambayo tumekuwa nayo ya Katiba, iwe ikiendesha wakati kwa wakati. Mnaona shida ambazo

zimekuweco, mara watu hawajui hivi wengine wanasema hawajafundishwa, mara mnasema pesa hakuna, kuna wengine nimekutana nao wanalia wanasema hata wanatembea kwa miguu hawajapata hata ndururu, hii ni kwa kuwa kulikuwa hakuna long term plan. Ikiwa civic education itakuweco after a certain tukiwa karibu katika uchaguzi. One year earlier wale wanahusika na civic education wanaingia uwanjani wanafundisha wananchi. Thank you very much.

**Com. Asiyu:** Asante sana mzee. Umeongea vizuri naona hakuna swali, oh! Dr. Maranga ana swali.

**Com. Maranga:** Mzee niko na swali muhimu. La kwanza kabisa ni Local Government, kwa hiyo umesema ungetaka kuwe na speaker wa Local Authorities, ile council. Sasa unataka kutoa speaker ndio muwe na badala ya clerk to the maybe County Council ama kwa County Council ama kwa ...

**Mr. Mativo:** Iwe ni running of the council.

**Com. Maranga:** Kwa hivyo mnataka kuongoza kama bunge?

**Mr. Mativo:** Partly yes.

**Com. Maranga:** Partly yes? No, now I want you to be clear. Do you want a parliament at the Local Authority level?

**Mr. Mativo:** Yes, yes a parliament

**Com. Maranga:** A small parliament.

**Mr. Mativo:** Ambayo inaendesha mambo yao.

**Com. Maranga:** Okey, question number two, umesema maana ya political parties. Unasema eti ni lazima wawe na registration ya one million. Sasa hukuniambia kama ni watu ama ni registered voters.

**Mr. Mativo:** Ni watu.

**Com. Maranga:** Watu, thank you.

**Com. Kangu:** Na bwana councillor umesema Local Authorities ziwe autonomous. Hukufafanua maana ya hiyo itakuwa ni hiyo kazi zake zitakuwa nini na nini na zile zinabaki kwa Central Government...ngoja tu Nitamaliza ushike yote, zile zinabaki kwa Central Government ni gani. Ukasema tena Local Authorities, revenue zake zipeanwe kwa Central Government only 25%, na

hukusema ni which revenue, which taxes zitakuwa raised na Local Authorities and which ones zitakuwa raised by the Central Government.

Ya tatu, unasema Local Authorities zipeanwe only 25% to the Central Government but at the same time unataka mshahara ya ma-councillors ilipwe kutoka kwa consolidated fund. Sasa ikiwa council zina-retain more money why should the consolidated fund which receives only 25% iwe ndio inalipa mishahara ya Councilors?

**Mr. Mativo:** One, ikiwa autonomous Local Authority ikiwa autonomous na ni kama zilikuwa autonomous before 1974, ilikuwa waalimu wanalipwa na Local Authority, hospitali ilikuwa katika Local Authority, mambo mengine yote na ilikuwa na GDP. So, hii revenue ambayo inatoka humu katika province, market, minerals, coffee, pyrethrum na vitu kama hivyo vyote viwe mikononi bila mkono wa Central Government, yote inaingia hapo kwa Local Authorities. Wakiwa namna hiyo utakuta wanaendelea vizuri na pesa watapata za kuendesha council bila wasi wasi. Watatengeneza barabara watangeneza kila kitu na pengine hata health centers kama vile tunasema ziwe chini ya Local Authorities.

**Com. Kangu:** Na hiyo wakati unasema mimi najua kweli Local Authorities zilikuwa na nguvu mingi na kazi mingi. Zilikuwa hata zinaruhusiwa kuitisha ile inaitwa graduated personal tax, kutoka kwa kila mtu. Hizo zote zikaondolewa, unataka zirudishwe ama namna gani.

**Mr. Mativo:** Hazitarudishwa, vile vile tunapata V.A.T ambayo inaingizwa katika Serikali, itakuwa katika Local Authority. Na taxation, moderlity yake itatengenezwa, itakuwa namna gani.

**Com. Kangu:** Local Authorities zenyewe tuko nazo saa hii zina a lot of confusion kwa sababu kuna municipal councils, tuna city councils tuna Town Councils, sijui urban councils, County Councils, unataka tuendeleo na structure hiyo ama tutapanga Local Authorities za aina gani.

**Mr. Mativo:** Tuwe na Local Authority kutoka 1974 or 5 zilikuwa zinaenda kisiasa. Unakuja hapa, market ambao haiwezi fanya sewage inaambiwa hiyo imekuwa promoted inakuwa Urban Council, town council, inaingia katika nchi as it wish. Pili, inakuwa marafiki wawe the big man, the big boss. Unachukua watu ambao pengine hawajaenda skuli kwa maana wanakuimba, unawaweka hapa halafu unasema niletee kitu, lazima ziwe restructured. Iwe hakuna zile zimejaa. Hata juzi Electoral Commission imepunguzwa number of councilors. For your information Wajir iko na a hundred and four councilors na wafanyi kazi ni themanini. Now, who is who?

**Com. Kangu:** Sijamaliza, wewe ni mzee umezungumzia hata mambo imekuweco 1963 na wakati imefika majimbo unasema majimbo itagawanya nchi, Wakamba pengine watafukuzwa Shimba Hills na mambo kama hivyo. Wakati tulikuwa na majimbo 1963 kama haijaondolewa 1964, ilileta haya mambo tunayosema ama haya mambo ya watu kufukuzwa ni mambo imeletwa na

wanasiasa whom we should deal with and just choose a good system?

**Mr. Mativo:** For your information mini nilikuwa Mombasa na nilipigania kiti cha senate 1963. Nikaanguka anyway for your information. President wa jimbo alikuwa Ngala. Wale watu wa coast walikuwa wanakuta by that term, sorry to mention kikuyu ndio walikuwa wanafagia the whole town. Kazi hiyo ilikuwa haitakikani na mtu mwingine. Mtu anakuja anachukua ile kifagio anamwambia hata sisi tunajua kufagia, nendeni kwenu, wabara kwao, hata sisi tunajua kufagia. Anafagia na mshahara hapati. Anafagia yeye na mshahara mwisho wa mwezi anaenda kupata yule mtu. Ikawa imepitishwa katika coast province regional assembly hakuna mtu ataandikwa kutoka any other province. Yaani nakwambia hiyo practical.

**Com. Kangu:** Nieleze ningetaka kujua hiyo historia.

**Mr. Mativo:** Sasa ikawa kwa kuwa partly ilikuwa ni njia moja ya kunyakua uhuru. Ikawa sasa tumefika majimbo ya bure. Lakini ile doctrine, ile iliyowekwa ya majimbo, ingali inafanya kazi. Leo leo tukichaguana katika KANU, unasikia na Eastern, na Nyanza, na coast, na kwetu, tukianza kuchaguana hapa hapa, utanza kusikia kwangu ni pale, utanza kusikia wa kwetu ni nani? Imeingia katika bongo za watu mpaka tunakuwa hata sasa on the regions na iliyoko ni kuondolewa katika Katiba.

**Com. Kangu:** Na sasa shida yenye tuko nayo kwa sasa, wakenya wengi ukisikia wakizungumza shida tuko nayo wanasema nguvu zote zimewekwa mahali pamoja, saa ingine kwa mkono ya mtu mmoja ndio hata waKenya ndio hata waKenya wamefika kiwango unasikia sasa it is our turn, kikuyus have had their turn, the kalenjins have had their turn it is now our turn. Sasa watu wanalia na sababu hiyo ni kwamba nguvu zote tumeweka mahali pamoja Central Government inakuwa ukipata nafasi it is your turn unaweza kuchukua everything unaacha wengine bure. Shida hii tutatatia namna gani?

**Mr. Mativo:** Hii imekuwa ya Local Authority. Nyinyi Machakos mkiwa na autonomous yenu makuoni muwe na autonomous ya Local Authority na embu mharibu shauri yenu. You must work hard muone mmeandika watu na mmetengeneza na hakuna mtu ata-interfere na nyinyi, hakuna jambo lolote lakini sauti iko katika Central Government.

**Com. Kangu:** Na hii Local Authority unasema, hatutafika kiwango watu wa Mombasa waseme tutaandika watu huku kwetu tusiandike wa nje.

**Mr. Mativo:** That is obvious.

**Com. Kangu:** Wanaandika wa kwao, so how are they different with majimbo then.

**Mr. Mativo:** Inaangalia Mombasa itakuwa namna gani, Nairobi itakuwa namna gani, Kisumu itakuwa namna gani, tutakuwaje Kenya ikiwa tunatoka Machakos mpaka tunafika Nairobi?

**Com. Asiyu:** Wewe ndio umetuambia.

**Com. Maranga:** Mimi mzee naona com. Kangu anauliza swali. Anasema tutafanyeje ili tuweze kupatia watu nguvu katika sehemu zao bila kubagua wanaKenya. Hiyo ndio swali anauliza. Yaani mtu anaweza kuwa mluhya anaandikwa Machakos lakini authority nguvu iko Machakos. Tunaelewana? Nafikiri hiyo ndio swali anauliza, ile sasa watu wa coast walikuwa wamepitisha, hiyo ilikuwa makosa, kusema eti mtu mwingine wa Kenya asifanye kazi Mombasa. Tumelewana? Mnaweza kuwa hapa nyinyi Wakamba eti mnakataa watu wengine lakini hamna watu wa kuchonga chuma ambao wanaweza kutengeneza kazi fulani. Tunaelewana? Lakini ndio tunauliza, itakuwezekanaje ili tuweze tukapeana nguvu kwa sehemu kama Machakos, district kama nini hiyo ndiyo maoni tunataka utupe.

**Mr. Mativo:** Tuko na Serikali kuu. Pale nilichagua President, nilijua wewe umejua President hawezi kuwa mahali ambapo hakuna Serikali kuu. Tuko na Serikali kuu ambayo iko mahali inaangalia mambo ya Central Bank. Inaangalia mambo ya port, inaangalia mambo ya security, inaangalia mambo mengine ambayo yanahusika katika nchi. Security haiwezi kuachiwa Machakos, security lazima iachiwe Kenya. Port ya Mombasa hatuwezi kuacha iwe ya watu wa pwani? Lazima tuwe katika Kenya, airport.

**Com. Asiyu:** Mzee vile unaulizwa ni hivi, hata sasa tuna huo huo mpango, lakini kuna shida kubwa katika Kenya, kwa maana minister kama ni wa works ana uwezo wa kuchukua pesa ilikuwa imeandikwa kutengeneza njia kutoka Masii kuenda pande hiyo ya Kitui apeleke kwao itengeneze njia ya kwao, na wewe huna la kufanya kwa maana ana hiyo haki na nguvu ya kufanya hivyo. Sasa utuambie, ni mpango gani inaweza, utusaidie tafadhali, tunaweza kuweka mpango gani ile mali ya umma iende kwa wananchi bila ya kuchukuliwa huku juu na wakubwa kupelekwa kwao na wengine wasio pale wanakosa huduma hizo.

**Com. Kangu:** Na nikiongezea tupate coffee inatoka Central Province, lakini kwa sababu ya Central Government, watu wanawekwa ku-manage coffee board, hawatoki central Province. They don't care about coffee. They run down the whole thing na wakulima wa coffee wanaumia. Because Central Government ukiwa nayo you can control everything everywhere. How do we deal with this/

**Mr. Mativo:** Hapo, tulipokuwa tuna autonomous ya Local Authority haikupi nafasi ya everything, tutakuja tukae chini tuseme this is want. Hii 25% niliyokupa kule ya collection ni ya ku-maintain the Central Government katika mambo yale ambayo nimetajataja, na ndiyo hiyo nilikuwa nikikujibu ya kwamba 25% ninakupa ili ulipe my Councilors. 25% ya income yangu ili ulipe the councilors from the Consolidated Funds na nimekujibu hivyo. Kwa hivyo ikiwa the Local Authority iko hapa iko na power, ina powers na ina nguvu ya kutafuta resources zao ya kutafuta management yao, hatuna daktari tutakuja Kisumu tutafute daktari hakuna engineer tutakuja Coast Province tukatafute engineer. So, through that, tutakuwa na autonomous na tunaweza kuzungumza na ...

**Com. Asiyu:** Kwa wakati huu, na unajua kwa kweli, kuna nchi zingine zimekuwa zaidi, zina lami zina mashule ya ajabu, zina mahospitali, kwa maana watu wakubwa walitoka upande hizo na pande zingine hakuna kitu. Wewe utusaidie tuandike Katiba ambayo itaangalia pande zote za Kenya, tufanye namna gani, tuandike namna gani?

**Mr. Mativo:** Tunataka Commission independent ambayo itaangalia distribution ya hizi pesa ambazo ni za Central Government, independent ambayo haiwezi kuingiliwa na President na mtu yeyote, an independent Commission of not less than 15 people.

**Com. Ayonga:** Ngoja kabla hujatoka, mimi nilitaka tu kukusaidia mzee. Unaona hawa watatu maswali ndio hayo, ulikuwa hukujitayarisha na haya maswali na kwa hivyo you need breathing space. Mimi sasa nataka nikuulize tu swali lile jororo maji tu, to finish off. Ulisema hii Katiba iandikwe in English, Kiswahilina Kikamba, I know uliposema Kikamba, hukusema itakomea hapo. In Kikamba means and other vernaculars?

**Mr. Mativo:** Yeah, kama the bible imeandikwa na kijaluo, na Kikamba na kiturkana, kwa nini si Katiba?

**Com. Ayonga:** Basi ambacho ulitaka kusema ni kwamba iandikwe kwa lugha zote za kenya. Asante ni hiyo tu.

**Com. Maranga:** Mzee nauliza swali la mwisho na unijibu vizuri, wewe ulisema hivi, mimi kama Wilson Mativo nimekataa kata kata sitaki majimbo lakini wakati unasema ati watu wa Machakos ndio wataajiriwa kazi tukiwa na autonomy ya Local Authority, hiyo inamaanisha hiyo ni majimbo kwa sababu wewe hutaki watu wengine unasema watu wanatoka hapa ama tuseme watu wa area hii ya Muuma Andu kwa mfano watasema hatutaki mtu kutoka Woote, hatutaki mtu kutoka Masii, hatutaki mtu kutoka Machakos, tunataka watu wa area hii sasa ndio watafanya nini, watapewa kazi. Si hiyo ni majimbo?

**Mr. Mativo:** Sio majimbo. Ni nyumbani.

**Com. Asiyu:** Asante sana mzee, tumekusumbua sana kwa maana wewe ni mtu mzee na una ujuzi mwingi na tulitaka kujifunza kutoka... hebu tunyamaze tafadhali. Tulitaka kujifunza kutoka kwako mzee ndio tujue tutaandika Katiba mpya namna gani na tulijifunza mambo mengi sana kutoka kwako. Tunakupua asante sana. Sasa namuliza bwana Samson Nguli aje na afuatwe na Dominic Kitilu. Tafadhali useme kwa kifupi mzee tuko na watu zaidi ya sitini wanataka kuongea na itakuwa ni vibaya sana kama wataenda bila kuongea kwa hivyo ongea tu kifupi, yale mambo ya muhimu tu. Naona umeandika tayari. Asante.

**Mr. Muteti:** Na ninaanza na hii mambo ya mahindi.

**Com. Ayonga:** Jina tafadhali.

**Mr. Muteti:** Samson Muteti, hii mambo ya farm produce ambayo ni juu ya mahindi, imekuwa kidogo, ni mbaya kwetu hapa na njia ya highlands. Mahindi yote ikipatikana, Board of Kenya Cereal Board inakimbilia highlands inasahau the arid areas kama hapa na Makueni, na wako na mahindi ambayo inaweza kununuliwa ni wale ili mkulima apate pesa ya kumsaidia. Wana-concentrate na highlands pekee yake.

**Com. Asiyu:** Unapendekeza namna gani?

**Mr. Muteti:** Napendekeza Katiba itambue fair distribution of purchase of farm products, mahindi.

Ile ingine, ni hapa kwa administration. Kuna shida kidogo kwa hii mambo ya democracy. Watu wameitumia mpaka wakasema ya kwamba chief akiitana watu wasije mtu anaanza kwenda kazi yake, kwa sababu hiyo democracy wanasema mimi ni upande wa DP... Katiba inaweza kuweka kitu kidogo ndani ya administration ya kwamba wanaweza kuita watu na wakuje bila ya kufanyiwa kosa lakini iko lazima wakuje na waambiwe ni kitu gani inaendelea kwa Serikali na waeleze kwa sababu ya hiyo kukatalia nyumbani.

**Mr. Muteti:** Wakati ya National days zile flag za Serikali, unaambia mtu aweke kwa duka, naye anakwambia, mimi apana wa chama cha Serikali ile iko, ile democracia imezidi kuwa mbaya. Kwa hivyo ile heshima ya Nation days haiko.

Jambo lingine, ni hii taabu ya DO, wanataabu sana. Utapata DO hana nyumba, raia wanaambiwa wachange pesa wanjenge nyumba. Serikali haiwezi ianze ile budget yetu ya mwezi wa sita or anything like that, inaweza kuspare some money kwa manyumba ya Mad.o halafu wanajengewa bila kusumbua wananchi.

**Com Hon Asiyu:** Jambo lingine.

